# Nipashe

Jumanne Januari 7, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581915

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


MPAMBANO CHADEMA

# Siri vita ya kugombea madaraka yafichuka



UKURASA 2

UKURASA WA 4

## Majaliwa awageukia wasimamizi miradi ya serikali



UKURASA WA 5

## Walimu kupimwa na wanafunzi uwezo masomo ya Sayansi



UKURASA WA 7

## JKCI kufuata wafanyakazi ofisini kupima moyo

TAASISI YA MOYO JAKAYA KIKWETE

# Shule msingi yaweka wanafunzi njiapanda

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimesalia siku tano pekee shule kufunguliwa kwa muhula wa kwanza wa mwaka 2025, wazazi na wanafunzi zaidi ya 600 wako njiapanda, baada ya moja ya shule kudaiwa kuwafukuza na kuwataka wahamishe wanafunzi.

Taharuki imeongezeka zaidi kutokana na uongozi wa shule kutoitisha kikao cha wazazi, badala yake mawasiliano yote yanafanyika kwa ujumbe mfupi wa maneno kupitia simu za kiganjani (SMS), kutoka shuleni kwenda kwa wazazi.

Baadhi ya wazazi waliozungumza na Nipashe jana, walisema badala ya shule kuitisha kikao, Ijumaa iliyopita Januari 3, 2025, Kaimu Mkuu wa Shule ya Rainbow, Denis Mbiro, alituma ujumbe kwa wazazi ukisisitiza wahamishie wanafunzi shule jirani.

**UJUMBE**

Ujumbe huo wa maneno 157, ambao mwandishi wa habari hii amefanikiwa kuuona na kuthibitishwa na Kaimu Mkuu wa Shule ya Rainbow unasomeka kwamba: "Ujumbe muhimu. Heri ya Mwaka Mpya."

"Uongozi wa Kanisa la Tanzania Presbyterian Church (TPC), unapenda kuwajulisha wazazi wa wanafunzi wa shule ya Hephzibah- upande wa

ENDELEA UKURASA 3

## Jenerali Muhoozi atishia kumuua Bob Wine

UKURASA 19

MICHEZO MZIZE ATABIRI BAO LAKE BORA AFRIKA UK.24

MAONI, UK.6



Mbowe



Lissu

# Siri vita ya kugombea madaraka yafichuka

**Na Elizabeth Zaya**

VITA ya madaraka ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), imeendelea kuvujisha siri yakiwamo yote ambayo yaliwahi kufanyika au kufanywa na viongozi wake kwenye vikao vyao vya ndani na vile vya nje ya chama hicho.

Tangu kuanza kwa vita hiyo, baada ya 'vigogo' wawili kutangaza nia ya kuwania nafasi ya uenyekiti taifa, siri za ndani ya chama hicho, zimekuwa zikitolewa kidogo kidogo kupitia kwa viongozi wenyewe katika mahojiano mbalimbali wanayofanya kwenye vyombo vya habari.

Vita hiyo pia, kwa takribani mwezi mmoja, imekuwa ikifanywa kwa njia mbalimbali ikiwamo kupitia mitandao ya kijamii, ikihusisha pande mbili za wafuasi wanaomuunga mkono Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wanaomuunga mkono, Tundu Lissu, ambaye kwa sasa ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho bara.

**KAULI YA LISSU JANA**

Jana Lissu akiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), akitokea nje ya nchi, alitoa siri nyingine ambayo alikuwa hajaisema hadharani.

Alisema kabla ya kutoka hadharani na kutangaza nia yake ya 'kukitaka' kiti cha uenyekiti, kulikuwa na mazungumzo mazito yaliyomhusisha yeye, Mbowe na viongozi wa dini kuhusu hatima ya nafasi mbili zinazotakiwa kugombewa ndani ya chama hicho.

Alisema mazungumzo hayo yalijikita kupanga nani awe Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na nani awe mgombea urais kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Alisema wakati yeye (Lissu) na Mbowe walipokutanishwa kwenye mazungumzo hayo, Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika alikuwapo.

Lissu alisema mazungumzo hayo yalifanyika kwa siku tatu mfululizo, hoja ikiwa ni kutafuta mwafaka katika kinyang`anyiro cha nafasi hizo mbili, ambazo viongozi hao wa dini walitaka wawili hao waamue.

Anaelezea zaidi kwamba yeye (Lissu), alifanya uamuzi wa kuwatamkia wazi viongozi hao wa dini kwamba anachotaka kugombea ni uenyekiti na kwamba kinyang`anyiro cha urais, anamwachia Mbowe.

Lissu alidai licha ya kueleza nia yake hiyo, lakini Mbowe kwa siku zote hizo tatu ambazo walikutanishwa, alieleza kwamba bado hajaamua chochote katika nafasi hizo zote mbili.

Kadhalika, Lissu alisema kuwa hata alipowaeleza wazi kuhusu nia yake hiyo, Mbowe hakukubaliana na uamuzi wake wa kutaka agombee nafasi hizo zote mbili, yaani uenyekiti na urais.

"Tulikutana kwa siku tatu, tukipatanishwa, tukizungumza juu ya hiki kinyang`anyiro na kwa siku tatu zote Mwenyekiti (Mbowe), alisema yeye hajaamua kugombea nafasi yoyote, Katibu Mkuu John Mnyika ni shahidi tukizungumza pamoja.

"Mwenyekiti hataki nitie nia, akiulizwa wewe...anasema mimi sijaamua, kwa siku tatu...nikaambiwa unasemaje, nikasema kwangu mimi suala la kuokoa hiki chama huko tunakoenda sio kuzuri, mimi niko tayari kugombea uenyekiti wa chama, urais nimwachie mwenyekiti, akakataa katakata (akimaamisha Mbowe)," alisema Lissu.

Lissu alisema baada ya mazungumzo hayo, hakuwahi tena kufanya mazungumzo yoyote na Mbowe.

"Kwa hiyo habari ya kusema mimi nataka yote, sijui siridhiki, si kitu chema kusema mwenyekiti amedanganya, lakini kwenye hili amedanganya," alisema Lissu.

"Amekataa nisigombee uenyekiti, amekataa nisigombee urais wakati yeye anasema hajaamua, eti anasema inabidi tuangalie kwanza, tupime upepo ila yeye hayuko tayari...kwa siku tatu," alisema.

Alisema walitakiwa kuzungumza na viongozi wa dini watatu, lakini walifanikiwa kuzungumza na kiongozi wa dini mmoja pekee.

"Nasikia huko wanasema huyo alipelekwa kwa viongozi wa dini...ni kwamba niliitwa na viongozi wa kidini watatu na nimekutana na mmoja tu...kwanza nilipokubali tu kukutana nao, Mwenyekiti 'aka-loose interest (akakosa hamu ya kuendelea)," alisema Lissu.

"Niliwekewa mgombea kwenye nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara, nikasaema aaaa... mimi nishindane na Ezekiel Wenje, ni bora nishindane na aliyemtuma."

Akizungumzia kuhusu hatua ya John Heche kutangaza kuwa upande wake, Lissu alisema anamtambua kama miongoni mwa wanachama ambao ni hazina kwa chama hicho.

Pia, alisema Heche ndiye alisababisha wao wakafahamu mambo mengi ambayo yalijadiliwa katika vikao vya maridhiano kati ya viongozi wa chama hicho na serikali.

"Heche ni moja ya hazina kubwa ya chama chetu, amekuwa mbunge wa chama chetu, amekuwa Mwenyekiti wa BAVICHA na Mjumbe wa Kamati Kuu. Sasa mimi nizungumzie nafasi yake ya Kamati Kuu na ubunge ambako nimefanya naye kazi kwa karibu.

"Heche alikuwa kwenye Kamati ya Maridhiano kama alivyosema, kama asingekuwa kwenye kamati hiyo ya maridhiano, tusingejua mambo mengi sana, kwa hiyo tutakapoandika historia sawa sawa ya haya maridhiano, tutamshukuru kwa kuwa, kwa sababu yake tulijua mambo mengi sana."

**MINYUKANO ILIVYOANZA**

Vita ya madaraka kati ya kundi la Mbowe na Lissu, iliyoanza kama minyukano kwenye mitandao ya kijamii, ambako siri za CHADEMA zilianza kuvujishwa na wanachama na wafuasi wa vigogo hao, lakini baadaye vigogo hao kwa nyakati tofauti wametoka hadharani na kueleza kile kinachoendelea.

Minyukano hiyo imekwishawaibua viongozi waandamizi, wakiwamo wagombea wa nafasi za uongozi kwenye uchaguzi uliopangwa kufanyika Januari 21, mwaka huu, katika ukumbi wa Mlimani City, mkoani Dar es Salaam.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Wenje, ambaye anagombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara, alitangaza kumuunga mkono Mbowe.

Mgombea mwingine wa nafasi hiyo, Heche, naye amejitokeza na kutangaza kumuunga mkono Lissu kwenye uchaguzi huo.

Heche na Wenje, wamekuwa wabunge kwa nyakati tofauti katika majimbo ya Tarime na Nyamagana, mtawalia.

Makada hao wote ni wajumbe wa Kamati Kuu na Mkutano Mkuu utakaochagua viongozi wakuu wa chama.

Kabla ya wanaowaunga mkono, Lissu kama mgombea katika nafasi hiyo ambayo imezua vita kali, ndiye alianza kwa kutoa mbele ya kamera kutoa baadhi ya siri au mambo yaliyokuwa yakiendelea ndani ya chama chake huku wenzake (Mbowe), akinyamaza kwa muda.

Hata hivyo, baadaye Mbowe naye alitoka hadharani na kuzungumza kidogo wakati akihojiwa hivi karibuni.

Katika mkutano wake baada ya kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti bara, Heche alisema kwamba anamuunga mkono Lissu kugombea nafasi hiyo kutokana na mrengo wake wa kutaka haki, ukweli na uwazi ndani ya chama hicho, huku akisema ataendelea kumtambua na kumheshimu Mbowe kama baba yake na mlezi wake kisiasa.

Uchaguzi wa viongozi wakuu wa chama hicho, unatarajia kufanyika Januari 21, mwaka huu na dirisha la kuchukua fomu kwa wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo lilifungwa juzi.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# Shule yaweka wanafunzi njiapanda

Na Mwandishi Wetu




ZIKIWA zimesalia siku tano pekee shule kufunguliwa kwa muhula wa kwanza wa mwaka 2025, wazazi na wanafunzi zaidi ya 600 wako njiapanda, baada ya moja ya shule kudaiwa kuwafukuza na kuwataka wahamishe wanafunzi.

Taharuki imeongezeka zaidi kutokana na uongozi wa shule kutoitisha kikao cha wazazi, badala yake mawasiliano yote yanafanyika kwa ujumbe mfupi wa maneno kupitia simu za kiganjani (SMS), kutoka shuleni kwenda kwa wazazi.

Baadhi ya wazazi waliozungumza na Nipashe jana, walisema badala ya shule kuitisha kikao, Ijumaa iliyopita Januari 3, 2025, Kaimu Mkuu wa Shule ya Rainbow, Denis Mbiro, alituma ujumbe kwa wazazi ukisisitiza wahamishie wanafunzi shule jirani.

**UJUMBE**

Ujumbe huo wa maneno 157, ambao mwandishi wa habari hii amefanikiwa kuuona na kuthibitishwa na Kaimu Mkuu wa Shule ya Rainbow unasomeka kwamba: "Ujumbe muhimu. Heri ya Mwaka Mpya."

"Uongozi wa Kanisa la Tanzania Presbyterian Church (TPC), unapenda kuwajulisha wazazi wa wanafunzi wa shule ya Hephzibah- upande wa shule ya msingi kuwa, tayari umeshafikia makubaliano na shule mbili, ambazo ni Joyland International School inayopatikana upande wa pili wa Fun City na Taneem Schools inayopatikana Toangoma kuwapokea wanafunzi wetu na kuendelea kupata huduma ya elimu mpaka ukarabati na ujenzi utakapokamilika.

Tunatambua wapo wazazi ambao walishapata shule za watoto wao kuendelea na masomo. Hivyo tunawaruhusu kuendelea pasipo kuleta mkanganyiko. Kwa wale ambao wamepata changamoto, wanaweza kuchagua moja kati ya hizi na mtoto atapokewa bila shida yoyote.

Shule zote mbili zitafunguliwa Jumatatu tarehe 13/1/2025. Tunaomba wazazi mfike kwa ajili ya taratibu za watoto kujiunga na shule.

Pia tumewasilisha majina ya wanafunzi wote katika shule zote mbili, mzazi unaweza kuchagua yeyote kati ya hizo. Mungu awabariki sana."

Awali, uongozi wa shule hiyo ya Awali na Msingi, Rainbow inayomilikiwa na Kanisa la Tanzania Presbyterian Church (TPC), ambayo ipo Kata ya Toangoma, wilayani Temeke, ilitangaza kufunga kwa mwaka mmoja na nusu kuanzia Januari mwaka huu, kwa kutuma SMS kwa wazazi na walezi wa wanafunzi.

Wakizungumza na gazeti hili jana, baadhi ya wazazi na walezi walisema baada ya kupokea ujumbe huo, waliomba uongozi uitishe kikao kutafuta njia ya kuwasaidia wanafunzi ili wasiathirike kimasomo, lakini uongozi umekataa kufanya hivyo.

Mzazi mwenye watoto wawili shuleni hapo, Magreth Laurent, alisema Desemba 6, mwaka jana, Meneja wa Shule za TPC, Mchungaji Hallington Kamanga, aliwatumia ujumbe mfupi akieleza sababu za kufunga shule kuwa ni ukarabati wa majengo.

Hata hivyo, alisema wazazi waliomba uongozi uitishe kikao cha pamoja na uongozi uliahidi kuitisha, bila kutekeleza.

"Hata tukiwapigia hawapokei na tulivyoenda kuomba kikao cha wazazi walisema watatupigia na badala yake wanatutumia meseji. Tunajiuliza serikali yetu inawaangalia watoto wa Tanzania wakinyanyaswa kiasi hiki kweli?" Alihoji.

Kwa mujibu wa wazazi hao, uongozi wa kanisa na wa shule hiyo, umekuwa na utaratibu wa kutuma ujumbe mfupi kwa wazazi na walezi kwa taarifa zinazohitaji mwafaka wa pamoja.

Ujumbe wa awali kutoka kwa Meneja wa Shule za TPC, Mchungaji Kamanga, ulisema shule ya Rainbow inafungwa kupisha ujenzi na maboresho ya majengo.

Mzazi mwingine, Dk. Lilian Isack, alisema wazazi waliomba wanafunzi hao wahamishiwe kwenye shule nyingine za TPC, pendekezo ambalo limepingwa na kanisa hilo.

"Ni kitu cha ajabu sana kwa kweli, tunajiuliza kwa nini wanawafukuza watoto kabisa? Wana shule nyingine, lakini hawawataki kabisa hawa watoto, tunajiuliza hawa ni wamishionari gani?"

Akizungumza na Nipashe jana, Mwalimu Mbiro alisema wamelazimika kuifunga shule hiyo ili kuboresha majengo na kuanza upya, kutokana na kupungukiwa na wanafunzi.

"Kanisa liliipokea shule mwaka jana ikiwa na idadi ndogo ya wanafunzi kiasi kwamba hatuwezi kuendelea kuiendesha na ndio maana tunaifunga kwa muda," alisema.

Alipoulizwa sababu za kutoitisha kikao cha wazazi badala ya kutuma ujumbe huo, Mbiro alijibu kwa kifupi kwamba hayo ni mawasiliano rasmi kutoka shuleni.

"Tuliwapa wazazi nafasi ya kuomba kujiunga na shule yetu nyingine kwa utaratibu wa wanafunzi kufanyiwa usaili ili watoto wanaofaulu wahamie kwetu, wapo waliofanikiwa. Kwa sasa tumefunga usaili na tumeingia makubaliano ya shule nyingine ambazo watoto wanaweza kuhamia hata bila usaili," alifafanua.

Alisema shule hiyo inafungwa baada ya kanisa kushinda kesi ya madai namba 28/2022, iliyofunguliwa na wachungaji Jung Hwan Kim na Sang Ok Nam, waliokuwa walalamikaji dhidi ya Bodi ya Wadhamini ya TPC, waliokuwa washtakiwa.

Baadhi ya wazazi waliiambia Nipashe kwamba uamuzi huo umekuja ghafla kwa kuwa Septemba, mwaka jana walisikia tetesi za shule hiyo kufungwa, lakini walipofuatilia kwa nyakati tofauti, uongozi wa shule na wa kanisa ulikanusha na kudai ni uzushi, huku wakiwataka waupuuze.

"Kufukuza mtoto wa darasa la kwanza bila huruma ni kutojali taifa la kesho. Tunaomba serikali iwasaidie watoto hawa wasio na hatia, wapate haki yao ya elimu," alisema Dk. Lilian.

**KESI**

Nakala ya hukumu ya kesi hiyo, ambayo Nipashe imeiona, ilitolewa Februari 5, mwaka huu na Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, John Nkwabi, aliyeirejesha shule mikononi mwa kanisa. Katika kesi hiyo, upande wa walalamikaji uliwakilishwa na Wakili Hamis Mbangwa na walalamikiwa uliwakilishwa na Wakili Paschal Kamala.

Hata hivyo, licha ya Kanisa kurejeshewa shule tangu Februari, uongozi wa kanisa haukuichukua shule hadi Septemba, mwaka jana.

Baadhi ya wazazi wamedai kuwa miezi minane ya TPC kutoingiza menejimenti mpya shuleni Rainbow sasa Hephzibah, ulilenga kuwawezesha walalamikaji, Jung Hwan Kim na Sang Ok Nam, kujenga shule mpya.

Mmoja wa wazazi mwenye wanafunzi shuleni hapo, ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alidai kuwa kilichotokea ni hujuma dhidi ya kizazi cha Tanzania kwa kuwa TPC ilishirikiana na menejimenti ya zamani kuwezesha ujenzi wa shule mpya katika eneo la Kisarawe II, lililoko Kata ya Kisarawe, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, ambayo imesajiliwa kwa jina la Rainbow Junior Christian.

Anasema kutokana na jina la Rainbow kuhamia Kisarawe II, TPC imelazimika kuibadilisha shule ya Toangoma jina na kuiita Hephzibah.

Wiki iliyopita, Kamishna wa Elimu Tanzania, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema kilichofanyika shuleni hapo ni kinyume cha utaratibu, kanuni na mwongozo wa shule, unaotaka haki ya mtoto ilindwe katika mazingira yoyote.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mtahabwa amewaelekeza wadhibiti ubora kwenda kukagua shule hiyo ili kubaini chanzo cha kufungwa kwake. Hata hivyo, jana mwandishi wa habari hii alimtafuta Kamishna bila mafanikio baada ya simu yake kuita bila kupokewa.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# Majaliwa awageukia wasimamizi miradi ya serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wasimamizi wa miradi inayotekelezwa na serikali ikiwamo ya elimu kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa ubora unaolingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Alitoa wito huo jana wakati wa ufunguzi wa Skuli ya Sekondari ya Makoba iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar.

Ufunguzi wa skuli hiyo ni sehemu ya shamrashamra kuelekea maadhimisho ya miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Alisema serikali imeendelea kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu ambayo kwa kiasi kikubwa imewezesha kuweka mazingira bora ya upatikanaji wa elimu ikiwamo ujenzi wa miundombinu.

Aidha, alisema katika kipindi cha miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameendelea kuipa hadhi sekta ya elimu kwa kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utoaji wa huduma za elimu.

"Sina shaka leo hii chini ya Jemedari Dk. Hussein Ali Mwinyi sote tunashuhudia mwendelezo wa hatua kubwa ya kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu nchini. Suala hili ni la kujivunia kwa kuwa ni matunda ya Mapinduzi ambayo sasa yanafikisha miaka 61 tangu kuasisiwa kwake".

Kadhalika, alisema serikali inayoongozwa na Mwinyi, imeendelea kufanya mageuzi makubwa ya elimu katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utoaji wa huduma za elimu nchini. "Mageuzi hayo ni pamoja na kutekeleza mtaala mpya wa umahiri utakaomwezesha mtoto kujifunza kwa vitendo na kumudu kasi kubwa ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia".

Alisema serikali imeendelea kutekeleza mipango, mikakati na kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kunakuwa na maendeleo kwenye sekta zote za kijamii ili kuleta tija inayotarajiwa kwa wananchi bila ubaguzi wa aina yoyote.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema kuwa Rais Dk. Mwinyi ameendeleza ari ya Waasisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha analeta mageuzi makubwa katika Sekta ya Elimu.

"Serikali hii iliahidi kuboresha miundombinu ya madarasa kwa shule za msingi kwa kujenga madarasa 1,000 na 500 kwa ngazi ya sekondari na mpaka sasa kwa ngazi ya msingi imejenga madarasa 2,893 na ngazi ya sekondari imejenga madarasa 1,917."

Ujenzi wa shule hiyo ambao umefikia asilimia 100 umegharimu Sh. bilioni 6.1 ambazo zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# Wanaoandaa maudhui yasiyofaa mtandaoni kukiona

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, amekemea wanaoandaa maudhui yasiyofaa na kuyasambaza mitandaoni.

Alisema wote watakaobainika kuandaa maudhui yasiyozingatia maadili, weledi na miongozo, watawajibishwa.

Alisema kumeibuka wimbi kubwa la waandaa maudhui hayo mitandaoni, ambalo linafanya kazi zake bila weledi jambo linaloleta athari kwa jamii.

"Waandaaji maudhui ya mtandaoni ni kundi muhimu ambalo, kazi zake zikizingatia weledi na miongozo ya kisera na sheria, hakika lina mchango chanya kwenye maendeleo na ustawi wa jamii kwa sekta zote.

"Hata hivyo, kumeibuka wimbi kubwa la waandaa maudhui hayo mtandaoni ambalo linafanya kazi zake bila weledi wa aina yoyote, jambo lenye athari kubwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii," alisema Dk. Dorothy.



Alitaja mfano wa maudhui machache ambayo yamesambazwa mitandaoni na kuwataka wayaondoe mara moja.

"Mathalani kwa uchache kabisa, hivi karibuni ameonekana mmoja akisambaza maudhui ya kuuza figo za mtoto, kuna mwingine anarusha maudhui ya kuandaa vinywaji na vyakula vichafu na kujitapa anawauzia wananchi wa Kariakoo na wengine wengi," alisema Dk. Dorothy.

Pia, alisema wapo wanaosambaza maudhui kuhusu fursa za kujipatia fedha kwa njia zisizoeleweka ili mradi waonekane wamesambaza.

"Ikumbukwe, jamii ya Watanzania inastahili kujipambanua kwa heshima na kuheshimu makundi ya rika mbalimbali yanayofanya shughuli mbalimbali za haki humo mitandaoni ambapo yanastahili heshima na staha.

"Kwa wale ambao tayari wamepakia maudhui kinyume na miongozo husika, wayaondoe mara moja kwa kuwa vyombo vyenye dhamana ya kusimamia uwajibikaji wa kisheria eneo hili viko kwenye sekta mbalimbali," alisema Dk. Dorothy.

Alitoa wito kwa waandaa maudhui wote, kuzingatia weledi na miongozo yote na kwamba kama kuna mtu hana elimu na ufahamu kuhusu kuandaa maudhui ya mitandaoni aache mara moja kwa sababu ataharibu na atawajibishwa.

"Wizara ninayoisimamia, itaendelea kuratibu ushirikiano wao kwenye kuwachukulia hatua watu wote wanaoandaa maudhui ya mitandaoni na kusambaza kinyume na sheria, jamii ni yetu wote, tuilinde ili iwe katika mazingira salama kwa malezi na makuzi ya watoto wetu wenyewe," alisema Dk. Dorothy.

# ACT yafungua mashauri 51 kupinga matokeo uchaguzi

**Na Halfani Chusi**

CHAMA Cha ACT-Wazalendo kimesema kimefungua mashauri ya uchaguzi 51 ya kupinga matokeo na mwenendo wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliofanyika Novemba, mwaka jana.

Kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa kwa umma na chama hicho jana, kesi hizo zimefunguliwa katika Mahakama za wilaya mbalimbali za Tanzania Bara na tayari hatua za awali ikiwamo wahusika kupokea wito wa mahakama kwa ajili ya kutajwa na kujibu mashauri zimeanza kufanyika.

Taarifa hiyo ilizitaja wilaya ambazo mashauri hayo yamefunguliwa kuwa ni Temeke, Lindi, Ilala, Momba, Mkuranga, Mafia, Kigoma na Kibiti.

"Chama cha ACT - Wazalendo kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kimejipanga kusimamia mashauri yote haya na tayari kimeshawapangia mawakili wake kesi watakazosimamia.

"Hatua ya kufungua mashauri haya ni mwendelezo wa dhamira ya chama kupigania demokrasia na haki za wananchi zilizoporwa wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, imani yetu kuwa kilichotokea kabla na siku ya uchaguzi hakikuwa uchaguzi bali uchafuzi na ahadi ya viongozi wetu ya kusimamia haki na demokrasia katika kila hatua," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo iliwataka wanachama na wapenzi wote wa demokrasia nchini kujitokeza kwa wingi wakati wa kesi hizo zinapoitwa mahakamani na chama kitaendelea kutoa taarifa ya kila hatua katika mwenendo wa mashauri hayo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA NJONBE, RUKWA, SONGWE NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA ZA NYASA, MBINGA, MJI WA MBINGA, WILAYA YA SONGEA NA MANISPAA YA SONGEA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na route ya tisa utafanyika katika Mikoa ya Njombe, Rukwa, songwe na Ruvuma katika Halmashauri ya Wilaya za Nyasa, Mbinga, Mji wa Mbinga, Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea tarehe 12 hadi 18 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumapili tarehe 12 hadi siku Jumamosi tarehe 18 Januari, 2025.
2. VITUO: Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika katika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa leo tarehe 03 Januari, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218312902

## Wajumbe CHAKUHAWATA wagomea mkutano mkuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADHI ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Kutetea na Kulinda Haki za walimu Tanzania (CHAKUHAWATA), wamegomea mkutano mkuu wa marekebisho ya katiba wakidai kuwa mchakato haujahusisha wanachama.

Katibu wa chama hicho Manispaa ya Mpanda, Nyavidunda Mhule, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo unaotarajiwa kufanyika leo na kesho jijini hapa.

Mhule, alisema walimu wanapaswa kuupinga mkutano huo kwa kuwa haujazingatia matakwa ya katiba ya chama wala maoni yao.

Alisema, wakati leo mkutano huo ukianza jijini hapa kwa muda wa siku mbili, wajumbe hawajapata hata nakala ya rasimu ya katiba inayofanyiwa marekebisho.

"Walimu tunapaswa kupinga mkutano huu kwa kuwa haujafuata katiba, lakini mabadiliko ya katiba hayajazingatia maoni ya wanachama hivyo kama yatapitishwa mabadiliko haya hayatakuwa na manufaa na wanachama bali maslahi binafsi ya viongozi," alisema.

Aidha, alisema licha ya jitihada walizofanya ili kuipata rasimu ya mabadiliko ya katiba hiyo, uongozi umegoma kuwapatia na badala yake walihoji wamesimamishwa kwenye nafasi zao.

"Mimi nimekwenda hadi ofisini kufuata rasimu ya katiba hiyo inayofanyiwa marekebisho sijapa, lakini badala yake viongozi wangu wamenisimamia kwenye nafasi yangu.

"Hivyo tunamuomba msajili wa vyama vya wafanyakazi kuvichunguza vyama hivi kwani vimekua vikikiuka sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na kuvunja katiba zilizowekwa na wanachama," alisema.

Akitoa ufafanuzi malalamiko hayo, Mwenyekiti wa CHAKUHAWATA Taifa, Emmanuel Helman, alisema mkutano huo umefuata taratibu zote na wajumbe hawapaswi kusikiliza maneno ya mtaani.

"Njia za kufikisha malalamiko kama haya zipo kikatiba badala ya kukimbilia kwenye vyombo vya habari, lakini sisi mkutano wetu upo kwani mamlaka zote zina taarifa nao.

"Aidha, tunachokwenda kufanya kwenye mkutano huu sio kupitisha katiba tu bali kupokea maoni ya wanachama wetu kipi kiwamo na kipi kiondolewe kwenye katiba yetu na tunatarajia kuwa na wajumbe wa mkutano mkuu takribani 476," alisema.




Mgombea wa nafasi ya Katibu wa Baraza la Wanawake-BAWACHA, Esther Dafi (wa pili kulia), akikabidhi fomu ya kugombea kinyang'anyiro hicho katika ofisi za CHADEMA Kanda ya Pwani, Dar es Salaam juzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Walimu kupimwa na wanafunzi uelewa masomo Sayansi, Tehama

**Na Grace Mwakalinga**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema itaanza utaratibu wa kuwapima na kufanya utafiti wa kufahamu matokeo ya mafunzo waliyoyatoa kwa walimu wa shule za sekondari wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), kwa kuwatumia wanafunzi ambao watapewa maswali ya kujibu kupima uelewa wao.

Kauli hiyo, ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia (Elimu), Dk. Charles Mahera, wakati akifungua mafunzo ya siku tano kwa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati pamoja na wathibiti ubora kutoka mikoa ya Simiyu na Mara yaliyofanyika wilayani Tarime.

Dk. Mahera, alisema kupitia Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP), wanatekeleza afua mbalimbali ikiwamo utoaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwa walimu wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Tehama.

Alisema katika kupima ubora na utekelezaji wa mafunzo hayo, wanaandaa utaratibu wa kuwapima walimu waliopatiwa mafunzo ili kuona tija kwa kuwatumia wanafunzi ambao wataulizwa maswali namna walivyonufaika.

"Serikali inatumia fedha nyingi kutoa mafunzo haya, lengo ni kuwajengea uwezo walimu wa sekondari wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Tehama mbinu zitakazowasaidia kuongeza uelewa kwa wanafunzi na kupenda masomo haya," alisema Dk. Mahera.

Aidha, wanakusudia kutoa mafunzo kwa walimu 40,000 Januari 2026 na hadi sasa 29,328 wamepata mafunzo hayo na kuimarisha ufanisi katika ufundishaji wa masomo hayo muhimu.

"Katika awamu hii, walimu 7,940 wanatarajiwa kufaidika na mafunzo haya, ikiwa ni hatua muhimu katika kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji," alisema Dk. Mahera.

Mratibu wa Mradi wa SEQUIP, Dk. Nicholaus Gati, alisema kuwa mradi umefanikiwa kwa asilimia 85 ya fedha zilizotengwa na malengo ya mradi yanajikita kuhakikisha wanafunzi, hususan wa kike, wanapata elimu ya sekondari na kumaliza masomo yao kwa mafanikio.

Alisema, wamejikita kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali (Tehama) na kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wa kike ili kushiriki kikamilifu katika elimu ya sekondari.

Mkurugenzi wa Ualimu, Dk. Huruma Mageni, alisema kupitia SEQUIP, walimu wamefundishwa kutumia mbinu za kisasa na changamshi ambazo zinakuza ubunifu na ufanisi katika ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati, na Tehama.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Tarime, Eliud Myovela, alisema matumizi ya Tehama yataongeza ufanisi katika ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufikia malengo yao kwa urahisi zaidi.

Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule kutoka Halmashauri ya Mji wa Bunda, Mwalimu Paulina Makolo, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuboresha mbinu zao za ufundishaji na kuongeza ufanisi wa wanafunzi katika masomo ya Sayansi, Hisabati na Tehama.

# Asilimia 59 majeruhi MOI ajali za barabarani

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI), imesema asilimia 59 ya majeruhi waliopokewa kwenye taasisi hiyo mwaka jana wanatokana na ajali za barabarani.

Imesema majeruhi wameongezeka kutoka 7,797 mwaka 2023 hadi wagonjwa 8,202 Desemba, mwaka jana sawa na ongezeko la majeruhi 405 sawa na asilimia 5.2.

Kaimu Meneja wa Kitengo cha Utafiti, Elimu na Ushauri MOI, Joshua Ngahyoma, alisema hayo alipozungumza kuhusu majeruhi wanaopokewa kwenye taasisi hiyo.

Ngahyoma alisema miongoni mwa wagonjwa hao, 3,350 ambao ni sawa na asilimia 41 wametokana na aina zingine za ajali, ikiwamo kuanguka huku 4,852 sawa na asilimia 59 wakitokana na ajali za barabarani.

"Januari hadi Desemba (2024) tumepokea wagonjwa 8,202 katika kitengo cha dharura, kati ya hao majeruhi wa ajali barabarani ni 4,852 sawa na asilimia 59, kati yao asilimia 21 ni ajali za magari na asilimia 38 ni ajali za bodaboda," alisema.

Akifafanua kuhusu wagonjwa waliotokana na ajali za barabarani, Ngahyoma alisema majeruhi 3,105 walitokana na ajali za bodaboda na 1,747 ajali za magari.

"Majeruhi 1,397 sawa na asilimia 45 ni madereva bodaboda, 963 sawa na asilimia 31 ni abiria wa bodaboda na 745 sawa na asilimia 24 ya majeruhi waliosababishwa na bodaboda kwa watembea kwa miguu," alisema.

Ngahyoma alisema baadhi ya wagonjwa ambao wamepata majeraha madogo ambayo hayakuhitaji upasuaji, walihudumiwa katika kitengo cha dharura.

"Wagonjwa ambao wamepata majeraha madogo ambayo hayakuhitaji upasuaji walikuwa 2,957 sawa na asilimia 36 ya wagonjwa wote waliohudumiwa katika kitengo cha dharura," alisema.

"Waliopata majeraha makubwa walikuwa 5,245 sawa na asilimia 64 ya wagonjwa wote waliohudumiwa katika kitengo cha dharura, wagonjwa 2,610 sawa na asilimia 50 walifanyiwa upasuaji wa dharura ndani ya saa 24 na wagonjwa 427 sawa na asilimia nane walipata huduma ya uangalizi wa karibu katika vyumba vya wagonjwa mahututi," aliongeza.

Alisema wagonjwa wote ambao wamefikishwa MOI wamepata majeraha ya kumia vichwa, migongo, kuvunjika mifupa mirefu, kukatika miguu, kuvunjika nyonga pamoja na vidonda vikubwa ambavyo vinasababishwa na ajali hizo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkutano Wakuu wa Nchi Afrika kuridhia upatikanaji nishati safi

**TANZANIA** inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika Januari 27, kuhusu nishati na unatarajia kuridhia na kusaini mpango mahsusi wa nishati Afrika, kuidhinisha awamu ya kwanza ya Mipango ya Kitaifa ya Nishati kwa kipindi cha 2025 hadi 2030 na kupitisha tamko la Dar es Salaam.

Mambo hayo yatakayofanyika katika mkutano huo, yatasaidia kuweka ramani ya kimkakati kwa maendeleo ya nishati barani Afrika yenye lengo la kukuza upatikanaji wa nishati endelevu na ya haki kwa wote.

Nchi 14, ikiwamo Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Nigeria, Zambia na Senegal, zitashiriki katika mpango huo wa kuboresha upatikanaji wa nishati na uhakika wa umeme katika maeneo yao.

Tamko la Dar es Salaam litasaidia kuainisha maono ya pamoja ya Afrika kuhusu maendeleo ya nishati endelevu na litakuwa mwongozo wa kuendeleza nishati mbadala, kuboresha miundombinu na kuhakikisha usawa wa upatikanaji wa nishati barani kote.

Mkutano huo unalenga kuleta pamoja marais wa Afrika na wadau mbalimbali ili kuhamasisha mabadiliko katika sekta ya nishati barani Afrika na jumla ya watu 1,500 wanatarajiwa kushiriki katika mkutano huo.

Mkakati wa nchi hizo kwa sasa ni kuja na mpango mahsusi ujulikanao kama 'mission 300' unaolenga kuweka mkazo kwenye kuharakisha matumizi ya nishati safi, endelevu na nafuu kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

Mpango huo unalenga kupunguza pengo la upatikanaji wa umeme barani Afrika kwa kupanua miundombinu ya nishati katika maeneo ambayo hayajafikiwa.

Fahari ya Tanzania ni kuwa mwenyeji wa mkutano huo, kama kiongozi wa kuendeleza nishati mbadala barani Afrika.

Rais Samia Suluhu Hassan ameufanya uongozi wake wa kimkakati katika kuendeleza miradi ya nishati safi, na juhudi zake zimelifanya taifa kuwa mstari wa mbele kupigania nishati safi ya kupikia na suluhisho endelevu la umeme.

Juhudi za kidiplomasia za Rais Samia zimeiweka Tanzania katika nafasi ya kipekee katika mazungumzo ya nishati barani Afrika.

Majadiliano ya mkutano huo yatagusia masuala muhimu ikiwamo maendeleo ya vyanzo vya nishati mbadala, upanuzi wa upatikanaji wa umeme vijijini na mijini na uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda afya ya umma na mazingira.

Alisema, kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia, Tanzania inalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya kaya zinapata suluhisho la nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Tanzania katika kuongeza upatikanaji wa umeme vijijini, zaidi ya asilimia 99 ya vijiji sasa vina nishati hiyo, huku zaidi ya vitongoji 32,000 vikiwa vimeunganishwa na gridi ya taifa na mafanikio hayo yameleta maboresho makubwa katika sekta za afya, elimu na uchumi nchini, na kutoa msingi wa ukuaji zaidi.


Mkutano huo pia utatoa jukwaa kwa viongozi wa Afrika kutia saini makubaliano muhimu yatakayobadilisha mazingira ya nishati barani.

Hii ni fursa ya kipekee kwa Tanzania kuimarisha nafasi yake duniani na kuonesha maendeleo yanayofanyika katika sekta ya nishati.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kufikia Desemba 2024, uzalishaji wa umeme Tanzania bara ulikuwa umefikia megawati 3,169.20.

Pia, upatikanaji wa umeme uliongezeka kutoka asilimia 14 mwaka 2011 hadi asilimia 78.4 mwaka 2020, kutokana na juhudi za Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Dawa ya wadanganyifu mitihani ni kuwajibishwa

**BARAZA** la Mitihani la Taifa (NECTA), limefuta matokeo yote ya wanafunzi 105 wa darasa la nne na 46 wa kidato cha pili kwa maelezo ya kufanya udanganyifu na kuandika matusi.

Mbali na hatua hiyo, NECTA pia imekifungia kituo cha Upimaji na Mitihani ya Taifa GoodWill cha Arusha kutokana na mkuu wa shule na baadhi ya walimu kuthibitika kufanya udanganyifu ili kusaidia wanafunzi.

Ni kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, akitangaza matokeo hayo wiki iliyopita, akifafanua kuwa yamefutwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(2)(j) cha Sheria ya Baraza la Mitihani pamoja na kifungu cha 30(2) (b) cha Kanuni za Mitihani za mwaka 2016.

Katika ufafanuzi wake wanafunzi hao 100 wa darasa la nne walifanya udanganyifu na watano waliandika matusi huku kwa kidato cha pili waliofanya udanganyifu ni 41 na watano waliandika matusi katika karatasi zao za majibu katika upimaji wa kitaifa wa kidato hicho.

Inaelezwa na Katibu Mkuu kuwa kati ya wanafunzi hao 100 waliofutiwa matokeo, 98 walipangwa na walimu wakuu kuwafanyia wanafunzi wenzao mitihani kwa maslahi binafsi.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba, kwa kuwa udanganyifu umekuwa wa miaka nenda miaka rudi, baraza lingeanzia kwa walimu hao kubaini mianya yote ya udanganyifu na kuidhibiti.

Walimu waliobainika kujihusisha na vitendo hivyo, wangebanwa ili wataje mbinu zote ambazo huwa zinatumika na kama wapo wengine zaidi nao watajwe waunganishwe katika kundi hilo.

Udanganyifu katika mitihani ni adui wa elimu ambaye bila kumchukulia hatua madhubuti, anaweza kusababisha madhara makubwa kwa miaka ya mbele ikiwamo nchi kukosa wataalamu bora wa fani mbalimbali.

> **Walimu waliobainika kujihusisha na vitendo hivyo, wangebanwa ili wataje mbinu zote ambazo huwa zinatumika na kama wapo wengine zaidi nao watajwe waunganishwe katika kundi hilo.**

Ninaeleza hivyo kwa sababu, wanaofanya udanganyifu wa mitihani na kufaulu kwa njia hiyo, hawawezi kufika mbali kielimu, kwani wanapokosa msaada wa udanganyifu si rahisi kufaulu.

Kwa kuwa udanganyifu huo umeshakemewa kwa muda mrefu lakini bado unaendelea, ninadhani hao waliobainika kushirikisha watoto wadogo wa darasa la nne katika mchezo huo, wangebanwa ili uwe mfano kwao na kwa wengine wenye nia ya kufanya uovu huo ili waache.

Watoto kama hao wa darasa la nne hawana wanachokifahamu zaidi ya kupokea kile wanachopewa. Hivyo, wale waliowashirikisha kufanya kitendo hicho ndio wanaotakiwa kuwajibishwa. Ninaungana na wale wanaosema kuwa elimu ni kama ibada haitaki najisi. Kwa kuwa watoto ni taifa la kesho, waachwe wafanye wenyewe kulingana na jinsi walivyojifunza bila kuongezewa udanganyifu.

Wakizoezwa kufanyiwa au kudanganya, matokeo yake na wao wataiga mtindo huo na kuuona kama sehemu ya maisha yao. Matokeo yake yanaweza kuwa ni kuongeza wadanganyifu kila sekta miaka ya baaadaye.

Mtindo huo katika mitihani usipodhibitiwa, unaweza kusababisha baadhi ya wanafunzi wakapungukiwa ari ya kupenda masomo na kupoteza uzalendo wao kwa taifa lao ambalo ndio wanalotarajia kulitumikia mara baada ya kuhitimu masomo yao.

Si sahihi kuwapo wanafunzi wanaofaulu kwa udanganyifu na wengine wakiumiza vichwa kwa kutumia akili zao. Ndio maana nikaeleza kuwa mtindo huo unaweza kusababisha wengine wakapunguza ari ya kusoma kwa kuwa wataona hata wakisoma kwa bidii wapo wenzao ambao watafaulu kirahisi kwa udanganyifu bila kuumiza vichwa.

HABARI KITAIFA

# DC awaonya waharibifu hifadhi pori Kilombero

**Na Idda Mushi,** KILOMBERO

MKUU wa Wilaya ya Kilombero, Wakili Dunstan Kiobya amewaonya watu watakaobainika kudhoofisha jitihada za kulinda na kuhifadhi Pori la Akiba Kilombero, mkoani Morogoro ambalo limetengwa maalum kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji, misitu na wanyamapori na upatikanaji wa maji katika mradi wa kimkakati wa Bwawa la Umeme la Nyerere (JNHPP).

Alisema hayo wilayani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa pori hilo.

Aliwaonya baadhi ya watu wanaowalaghai wananchi na kuendelea kulima na kuchunga mifugo ndani ya pori hilo na kuuza maeneo kwa ajili ya shughuli za kilimo kinyume na sheria kwa kuwa maeneo ya hifadhi hayaruhusiwi kwa shughuli zozote za kibinadamu isipokuwa zile zinazoruhusiwa kisheria.

"Kumebainika uwapo watu wanaowatapeli wananchi kwa kuwauzia maeneo ndani ya hifadhi ndio maana namwagiza Mkuu wa Polisi wilaya pamoja na Kamati ya Usalama ya wilaya kuendelea kufuatilia kwa ukaribu suala hili na wote watakaobainika kuwarubuni wananchi, kuwalaghai, kuwatapeli kwa njia moja ama nyingine wachukuliwe hatua kali za kisheria," alisema.

Aliwaasa viongozi na watendaji katika ngazi mbalimbali wilayani humo kuongeza ulinzi kwenye maeneo tengefu ya Pori la Akiba la Kilombero na kuweka utaratibu wa kuwapokea wananchi wanaohamia kutoka ndani ya hifadhi hiyo hasa wanaoingia kupitia maeneo ya pembezoni mwa hifadhi kama Idete, Mngeta, Mofu na Namawala.

Maeneo mengine ni Kalengakelu, Chombe, Chita, Chisano, Ching'anda, Mlimba, Utengule na jirani na hifadhi.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan ameonesha imani na nia nzuri kuhakikisha hifadhi yetu hii (Pori la akiba la Kilombero) lisiharibiwe na watu wachache badala yake kila mmoja ashiriki kulilinda kutokana na umuhimu wake hasa kwa uhifadhi na mazingira na kutupatia maji ya kutosha kwa matumizi mbalimbali ikiwamo ya uzalishaji wa umeme," alisisitiza Kiobya.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, Jamal Idrisa Abdul, alimshukuru Rais Samia kwa kulipandisha hadhi Pori la Akiba la Kilombero na kusisitiza kazi iliyobaki ni kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kutunza, kuilinda na kuihifadhi pamoja na kurejesha uasili wake.

Hadi sasa kazi wanayoendelea nayo ni kuhakikisha wananchi hawaendelezi shughuli zozote za kibinadamu katika hifadhi hiyo.

Kamanda wa Pori la Akiba Kilombero, Bigilamungu Kagoma, alisema tangu hifadhi hiyo ipandishwe hadhi, mamlaka hiyo imeendelea na uwekaji vigingi ili kuifanya mipaka ya hifadhi kuonekana vizuri na kutambulika wazi kwa wananchi.

"Mpaka sasa tumeshaweka zaidi ya vigingi 1,100 katika maeneo mbalimbali ya hifadhi," alisema Kagoma.



Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza kutoka Ofisi ya Kilimo, Ufugaji na Utunzaji Mazingira, Daimu Mmolosho (wa nne kulia), akiwa na maofisa wengine wameshika miti tayari kwa ajili ya upandaji katika kata ya Msalato, Dodoma jana, jumla ya miti 1,500 ilipandwa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Madaktari JKCI 'kuwasaka' wagonjwa wa moyo ofisini

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imeanzisha huduma ya kuwapima afya ya moyo wafanyakazi wanapokuwa ofisini.

Meneja Masoko wa JKCI, Irene Mbonde, alisema hayo wakati akizungumzia kuanzishwa huduma hiyo.

Alisema wameamua kuanzisha huduma hiyo baada ya kubaini kuwa baadhi ya watu wanashindwa kwenda kupima afya zao kwa kutingwa na majukumu yao ya kila siku.

"Tumebaini kuwa watu wengi wanafanya mazoezi bila kujua afya zao na wengine wanapata msongo wa mawazo wakiwa kazini, wengine wanaanguka na kupata matatizo mbalimbali kama kiharusi ndio maana tumeanzisha hii programu," alisema.

"Tumebaini kwamba watu wengi hawaji kupima kwa kuwa na majukumu mengi kwa hiyo tukiwafuata huko tutawarahisishia kupima afya zao za moyo walipo wakiwa wanaendelea na kazi zao ili wanaobainika kuwa na shida waanze matibabu mapema kabla ya hali kuwa mbaya," alisema.

Alisema programu hiyo itasaidia kupunguza gharama

**Alisema wameamua kuanzisha huduma hiyo baada ya kubaini kuwa baadhi ya watu wanashindwa kwenda kupima afya zao kwa kutingwa na majukumu yao ya kila siku.**

za matibabu kwa watu ambao wanagundua matatizo yao ya afya zao hali ikiwa mbaya kwa kuwa kupitia programu hiyo watabaini mapema na kupata tiba kwa gharama nafuu.

Alisema kampuni mbalimbali, taasisi za umma na binafsi zitakazohitaji huduma hiyo zinaweza kuwasiliana na uongozi wa taasisi hiyo ili kupata huduma kwa wafanyakazi wake.

Wakati huo, JKCI imewaalika wataalamu wa afya nchini kwenye mkutano wa kimataifa wa magonjwa ya moyo unaotarajiwa kufanyika wiki hii.

Taarifa ya JKCI ilisema jana kuwa kwenye mkutano huo mada mbalimbali zikiwamo za matibabu bobezi ya moyo kwa kutumia mtambo wa kisasa wa Cath lab pamoja na namna ya kuepuka magonjwa hayo zitatolewa.

Ilisema mada zingine zitakazotolewa ni pamoja na magonjwa ya moyo kwa watoto, huduma muhimu baada ya upasuaji wa moyo, uchunguzi bobezi wa moyo, upasuaji mkubwa wa moyo na mishipa ya damu, teknolojia ya akili bandia kwenye upasuaji wa moyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Serikali kuweka kipaumbele bajeti malisho ya mifugo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakusudia kuweka bajeti kila mwaka vipaumbele kwenye eneo la malisho ya mifugo na maji ili wafugaji wafuge kisasa wakiwa katika maeneo yao rasmi badala ya kuhamahama.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji alisema hayo wilayani Mvomero wakati wa kikao chake na viongozi wa Serikali ya Mkoa wa Morogoro, wakiwamo wa wilaya hiyo pamoja na baadhi ya wafugaji.

Aliwataka wakuu wa mikoa nchini kuhamasisha mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kuiwezesha serikali kuboresha miundombinu ya ufugaji.

Alisema mpango mkakati huo unalenga kuwaondolea adha wafugaji kutotembea muda mrefu kufuata mahitaji hayo muhimu kwa ajili ya mifugo yao.

"Tayari kwenye mpango huu tumeanzia Morogoro kuleta mbegu za malisho ya mifugo ili wafugaji wawe na maeneo yao rasmi kwa ajili ya kilimo cha malisho ya mifugo," alisema Dk. Kijaji.

Alisema katika mwaka wa fedha 2025/26, serikali itaanza utekelezaji wa mpango wa kuchimba visima na mabwawa ili kuwahudumia wafugaji na mifugo yao nchini.

Aidha, alisema vituo atamizi na mbegu bora za mifugo ndio chachu kwa Tanzania kuwa na nafasi kubwa ya kuuza mazao ya mifugo nje ya nchi na kuondokana na vikwazo vya kimataifa ambavyo imekuwa ikikabiliana navyo juu ya ubora wa mazao hayo yanapotakiwa katika nchi hizo.

Alimhakikishia Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, upatikanaji wa mbegu bora za malisho kwa ajili ya mashamba 1,200 ya wafugaji ambao wamekubali kujiunga kwenye kampeni ya Tutunzane Mvomero.

Alisema changamoto inayowakabili wafugaji wengi ni suala la malisho ya uhakika na maji hasa nyakati za kiangazi na kwamba wizara itahakikisha mbegu hizo zinapatikana ili mashamba ya wafugaji yapandwe kusaidia kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

"Huu mpango wa ugawaji wa mbegu za malisho ni kuunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye aliizindua kampeni hiyo Agosti 3, 2024 hivyo na sisi wizara tumesimama imara kwenye utekelezaji wake," alisema Waziri Dk. Kijaji.

Katika hatua nyingine, alimwagiza Naibu Katibu Mkuu wizara hiyo anayeshughulikia mifugo kufanya utafiti wa haraka ili kujenga kisima au bwawa katika kijiji cha Kambala kabla ya bajeti ya mwaka 2025/2026 ili wafugaji hao kuacha kufuata maji umbali mrefu na kusababisha migogoro baina yao na wakulima.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Nguli alisema upatikanaji wa mbegu za malisho pamoja na gharama za uchimbaji wa visima ni changamoto mojawapo katika utekelezaji wa kampeni hiyo ya Tutunzane Mvomero.

Nguli alisema wakati kampeni hiyo inaanza kutekelezwa kuna mashamba 379 ambayo yalipatiwa hati kwa ajili ya kupanda malisho ya mifugo.

Baadhi ya wafugaji akiwamo Chifu Kashu Moreto kwa nyakati tofauti waliipongeza serikali inavyowapambania wafugaji waweze kuleta mabadiliko kwa wafugaji huku ikiwahimiza kufuga kisasa na kuwasogezea huduma mbalimbali karibu na maeneo yao.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala (kulia), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo vyakula kwa watoto wenye uhitaji maalumu wa kituo cha Upendo Rehabilitation kilichopo Magomeni mkoani humo juzi. Msaada huo umetolewa na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Mtwara. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Watoto wakabidhiwa misaada zaidi ya mil. 8/-

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

SERIKALI mkoani Mtwara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekabidhi msaada mbalimbali kwa watoto zaidi ya 1,000 wenye mahitaji maalumu mkoani humo uliogharimu Sh. 8,049,000.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala, alisema anaamini moyo huo wa kuwashika mkono watoto wao utaendelea ili waendelee kupata faraja zaidi.

"Niwashukuru wadau wote ambao wameweza kushiriki kwa namna moja ama nyingine tunaamini moyo huu wa kuweza kuwashika mkono watoto wetu utaendelea ili waendelee kupata faraja zaidi," alisema Kanali Sawala.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kushiriki na makundi mbalimbali katika nyakati mbalimbali ikiwamo sikukuu za mwisho wa mwaka.

"Mheshimiwa Rais ameonesha njia ya namna na kushirikiana na kuwapa nafasi watoto wetu ambao wana mahitaji maalum waliyopo kwenye vituo ambao nao wanahitaji faraja kama wengine katika sikuu hizi za mwisho wa mwaka," alisema.

Mwalimu na mlezi kutoka kituo cha kulelea watoto cha Upendo Rehabilitation kilichopo Magomeni Manispaa ya Mtwara Mikindani, Sikudhani Ayubu, alimpongeza mkuu huyo wa mkoa kwa kuwapatia msaada huo kwa watoto hao.

Mmoja wa watoto hao wenye wahitaji maalum akiwamo Nurdini Abdallah kutoka kituo cha Rahaleo, aliushukuru uongozi kwa kuendelea kuwajali kwasababu mara nyingi wanapatiwa misaada na kufarijika.

Watoto waliopatiwa msaada huo ni kutoka kwenye vituo sita baadhi ya halmashauri ikiwamo ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, Wilaya ya Masasi na Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

## Dereva alivyofariki dunia ajali ya basi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

DEREVA Cuthbert Likaliko (58), mkazi wa Mkoa wa Pwani amefariki dunia papo hapo baada ya gari alilokuwa akilisafirisha kwenda nje ya nchi kugongana uso kwa uso na basi mali ya Kampuni ya Frester, mjini hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo Januari 4, mwaka huu majira ya saa 5:00 usiku kwenye makutano ya Barabara Kuu ya Singida-Mwanza eneo la Sabasaba mjini hapa.

Kakwale, alisema dereva huyo alifariki baada ya gari hilo alilokuwa akiendesha aina ya Toyota Canter akilisafirisha kugongana na basi hilo linalofanya safari zake kati ya Moshi mkoani Kilimanjaro na Geita.

Muuguzi kiongozi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida, Asha Kanpuni, alisema baada ya kupewa taarifa za ajali hiyo kitengo cha dharura cha hospitali hiyo kilifika eneo la tukio na kuchukua mwili wa marehemu.

Asha, alisema katika ajali hiyo hakukuwa na majeruhi wengine.

Alisema uchunguzi wa madaktari wa hospitali hiyo walibaini kuwa dereva huyo alikufa kutokana na kujeruhiwa vibaya sehemu za kichwani.

Madereva wa bodaboda katika eneo la Sabasaba walisema katika eneo hilo kumekuwa kukitokea ajali nyingi kutokana na madereva kutozingatia taa za usalama barabarani.

Elia Timothy, alisema katika eneo hilo usiku na mchana madereva wamekuwa hawazingatii taa za usalama barabarani na kusababisha ajali kutokea mara kwa mara.

Aliwaomba askari wa kikosi cha usalama barabarani kusimama katika eneo hilo muda wote ili kudhibiti madereva wazembe na kuepusha ajali zisizo za lazima.

**Asha, alisema katika ajali hiyo hakukuwa na majeruhi wengine.**



## Mamlaka za maji zakusanya mabilioni

Na Jaliwason Jasson, BABATI

MAMLAKA tatu za maji mkoani Manyara zimekusanya shilingi bilioni 2.3 kwa robo ya kwanza ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2024/25 kati ya shilingi bilioni 9.6 ya malengo zilizojiwekea.

Mamlaka hizo ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Mbulu na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kibaya.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA, Iddy Msuya wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha upande wa miradi ya maendeleo mamlaka hizo zilitenga Shilingi milioni 668, lakini serikali kuu imezitengea Shilingi bilioni 11.

Alisema licha ya kukusanya Shilingi Bilioni 2.3 kwa robo ya kwanza, mamlaka hizo zimetumia shilingi bilioni 2.6 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.

Alisema miradi inayoendelea kutekelezwa mwaka wa fedha 2024/25 itatumia shilingi bilioni 44.6 na ikikamilika itazitoa mamlaka za maji kwenye upatikanaji wa maji kwa asilimia 84 mpaka asilimia 95.

Mkurugenzi huyo, alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, mamlaka hizo zilikusanya shilingi bilioni 6.39.

"Pamoja na makusanyo hayo, serikali kuu ilitoa Sh. bilioni 30 badala ya ile Sh. bilioni 6 na matumizi kwa mamlaka tatu yalikuwa Bil.7.3," alisema Msuya.

Alieleza kuwa kiasi hicho cha Shilingi bilioni 30 zilizotolewa na serikali kuu zilisaidia kukamilisha miradi tofauti ya maji.

**Alisema kwa mwaka huu wa fedha upande wa miradi ya maendeleo mamlaka hizo zilitenga Shilingi milioni 668, lakini serikali kuu imezitengea Shilingi bilioni 11.**

# TIC yaagizwa kuwawezesha wawekezaji wazawa nchini

Na Jaliwason Jasson, BABATI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo amekiagiza Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) kuwaangalia wawekezaji wazawa kwa jicho la pekee ili wafanye uzalishaji kwa ufanisi.

Vilevile ameliagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Tume ya Ushindani nchini (FCC) kudhibiti bidhaa feki zinazozalishwa mitaani na kudumaza wawekezaji wazawa.

Mkumbo alitoa maagizo hayo jana mjini hapa baada ya kutembelea Kiwanda cha Mati Super Brands Limited kinachomilikiwa na mwekezaji mzawa, David Mulokozi.

"TIC wawekezaji kama hawa muwape jicho la pekee kila wanachohitaji wapewe ili waweze kufanya uwekezaji wao," alisema.

Alisema uwekezaji unaofanywa unasaidiwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika kutoka Bwawa la Julius Nyerere na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mji wa Babati (BAWASA) ambao ndio wanatoa huduma ya maji kwa mwekezaji huyo.

Kuhusu bidhaa feki lililoelezwa na Mkurugenzi Mulokozi, alisema wanalichukua kwa uzito mkubwa.

Prof. Mkumbo, alisema TBS na FCC wanatakiwa kuhakikisha wanadhibiti bidhaa feki kwa kuwa zinaathiri uchumi na upatikanaji wa kodi za serikali.

Alisema licha ya ubunifu anaofanya mwekezaji huyo wa kuboresha mifumo, anatakiwa kuhakikisha vijana wanapata ajira ili kusaidia serikali kupunguza wimbi hilo kuzagaa mitaani.

Alisema kuhusu hoja ya mabadiliko ya sheria kuwa na athari kibiashara, Mkumbo, alisema kuanzia mwezi ujao, wataanzisha chombo cha kusimamia masuala yote ya uwekezaji na sheria kubadilika.

"Mabadiliko ya mara kwa mara ya sera na sheria tunazifanyia kazi na serikali itaendelea kumuunga mkono mwekezaji ili afanikiwe," alisema.

Mulokozi, akitoa taarifa kwa waziri huyo, alisema ulipaji wa kodi umekuwa ukiongezeka kila mwaka.

Alisema mwaka 2022 walilipa Shilingi bilioni 7.7, mwaka juzi bilioni 7.9 na mwaka jana bilioni 8.

Alisema ameajiri wafanyakazi 269 kati ya hao, wa kudumu 147 na kawaida ni 122.

Mkurugenzi huyo, alisema changamoto waliyo nayo ni kukosa chupa kutoka Kiwanda cha Kioo Limited na kulazimika kuagiza bidhaa hiyo kutoka Kenya au Oman.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo (kulia), akisalimiana na mmoja wa wawekezaji mkoani Manyara, David Mulokozi, alipotembelea wawekezaji mkoani humo jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Wananchi Msitu wa Tembo kuunganishiwa barabara

Na Godfrey Mushi, SIMANJIRO

SERIKALI inatarajia kufungua mawasiliano ya barabara ya Langa/Mkuu na Ngorika-Ngage na kuziunganisha ili kupunguza adha ya kusafiri umbali mrefu wakazi wa Msitu wa Tembo wilayani hapa Mkoa wa Manyara.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Simanjiro, Naftari Chaula alitangaza mpango huo jana wakati wa ukaguzi wa utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa barabara wilayani hapa.

Kwa mujibu wa Chaula, barabara hiyo imekuwa ikikumbwa na mafuriko pamoja na sehemu nyingine kufungwa kutokana na kuwa na makorongo mengi yaliyosababishwa na mvua.

"Kwa mwaka huu wa fedha, tunatarajia kukamilisha ujenzi wa madaraja kwa zaidi ya asilimia 70, tayari mkandarasi yupo eneo la ujenzi akiendelea na uchimbaji na upangaji wa mawe.

"Ujenzi huu ukikamilika utafungua mawasiliano kati ya Kata ya Ngorika na Msitu wa Tembo na kuwezesha usafirishaji wa mazao ya uvuvi kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu," alisema na kuongeza kuwa:


"Wananchi wamekuwa wakipata shida sana katika shughuli za usafirishaji wa mazao ya uvuvi, bidhaa nyingine za kilimo na hata wa Ngorika kwenda Hospitali ya Kata ya Msitu wa Tembo na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC iliyoko Moshi, Kilimanjaro na kwingine kwa matibabu."

Kwa upande wao, wakazi wa kata hiyo wameishukuru serikali kupitia TARURA kwa kuwapelekea mradi huo kuwa utasaidia kuondoa changamoto walizokuwa wakikutana nazo.

Thomas Sokoine, Mkazi wa Kijiji cha Londoto, Kata ya Msitu wa Tembo, alisema kujengwa kwa daraja katika korongo hilo, kutasaidia wananchi wakiwamo watoto kuvuka upande wa pili.

Robert Juma, dereva wa lori, alisema barabara hiyo imekuwa na changamoto wakati wa mvua na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapelekea mradi huo wa ujenzi wa makalavati.

Jorum Yohana, Mkazi wa Msitu wa Tembo, alisema maeneo yao yalikuwa ni hatarishi kwao kutokana na kujaa maji kuleta adha kubwa kwa wananchi.



# Wanaoozesha wanafunzi kufungwa jela

Na Shaban Njia, KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita amesema atawafunga jela wazazi na walezi watakaobainika kuwaozesha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa tamaa za kujipatia mali.

Mboni, alisema hatua hiyo itaenda sambamba na wazazi na walezi watakaobainika kuwaficha watoto wenye ulemavu waliofikia umri wa kuanza darasa la awali, la kwanza kwa kosa la kuwakosesha haki ya kupata elimu.

Alitangaza mpango huo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake jinsi serikali ilivyojipanga kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za sekondari za Halmashauri ya Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama wanaanza masomo mwezi huu.

Mboni, alisema wameanzisha operesheni maalamu kuhakikisha wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaingia darasani na kuanza masomo yao kwa wakati.

Alisema serikali imetengeneza mazingira mazuri ya kusoma, hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kwenda shule kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa Mboni, katika Halmashauri ya Ushetu ilibainika kulikuwa na tatizo la wazazi kuwaoza wanafunzi na wakati mwingine kuwarubuni wafanye vibaya kwenye mitihani.

Alisema kwa sasa tatizo hilo halipo baada ya kudhibitiwa na kusalia Msalala na Manispaa ya Kahama kutoka na kuwapo kwa migodi midogo ya machimbo ya madini.

**Mkazi wa Nyihogo Manispaa ya Kahama, Hotesea Methord, alisema ugumu wa maisha chanzo cha wazazi wengi kuwaoza wanafunzi ili kupata fedha na ng'ombe na kujikwamua kiuchumi.**

“Katika Kata ya Ngogwa na Zongomela Manispaa ya Kahama kuna mabinti walikuwa katika harakati za kuozeshwa, tulipata taarifa kupitia operesheni tunayoifanya na kuzuia jaribio hilo. Niwaonye wazazi na walezi kutokuwa sehemu ya kukwamisha ndoto za elimu kwani sitawavumilia nitawafunga,” alisisitiza Mboni.

Kuhusu wanafunzi wa awali na darasa la kwanza, alisema utaratibu wa uandikishwaji unaendelea.

Mkazi wa Segese, Msalala Richard Godfrey alisema, maeneo ya wachimbaji wadogo wanafunzi wamekuwa wakiwekwa kinyumba, baadhi kupewa ujauzito na kubaki wakihangaika mitaani.

Mkazi wa Nyihogo Manispaa ya Kahama, Hotesea Methord, alisema ugumu wa maisha chanzo cha wazazi wengi kuwaoza wanafunzi ili kupata fedha na ng'ombe na kujikwamua kiuchumi.



Mkazi wa jijini Mwanza akikusanya samaki aina ya sato ili kuwaandaa kwa ajili ya kuwauza jana, baada ya kuwavuna kwa njia ya kisasa ya vizimba inayotumiwa ndani ya Ziwa Victoria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kipindupindu chalipuka Bunda

Na Vitus Audax

WAKAZI wa Wilaya ya Bunda mkoani Mara, wametakiwa kuchukua tahadhari kukabiliana na ugonjwa wa kipindipindu baada ya kuibuka katika Kijiji cha Mekomariro.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Salum Mtetela wakati akitangaza maazimio ya kikao cha kamati ya afya cha dharura ili kudhibiti kusambaa ugonjwa huo wilayani humo.

Mtetela ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, alisema miongoni mwa sababu zilizobainika kuwa chanzo kuibuka kwa ugonjwa huo ni wananchi kutozingatia matumizi sahihi ya vyoo.

Alisema asilimia kubwa ya kaya katika kijiji hicho hazina vyoo, wananchi wengi wanatumia maji si safi na salama kwa afya zao ya kwenye mabwawa.

Alisema kikao hicho kiliazimia uongozi wa kata na wilaya kuhakikisha kaya hizo zinajenga vyoo hadi kufikia Januari 10, mwaka huu na kufuata matumizi sahihi ya vyoo.

Alisema kikao hicho pia kimeazimia kusitisha mikusanyiko isiyokuwa ya lazima katika kijiji hicho na huduma ya chakula misibani, minada na migahawa kuanzia Jumamosi iliyopita.

“Kikao kimeelekeza Mamlaka ya Maji kuhakikisha inaboresha huduma ya maji katika kata hiyo na kuhakikisha wanachunguza na kutibu vyanzo rasmi vya maji vinavyotumiwa na wakazi wa eneo hilo,” alisema Mtelela.

Kadhalika, alisema kikao hicho kimeelekeza viongozi wa maeneo hayo kuendelea kutoa elimu ya afya na usafi wa mazingira mara kwa mara.

“Wananchi wote wilayani hapa wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa kuzingatia misingi ya usafi wa mazingira na vyakula ili kuepuka ugonjwa huo,” alisisitiza Mtelela.

## ‘Wananchi vijijini wahamasishwe kupikia gesi safi’

Na Shaban Njia, KAHAMA

MENEJA wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Magharibi, Walter Christopher amesema matumizi ya nishati chafu bado makubwa vijijini na kuwataka wananchi kuwa mstari wa mbele kuhamasishana kuhamia nishati safi.

Christopher alitoa rai hiyo juzi wilayani hapa wakati akifungua mafunzo kwa wadau wa nishati safi.

Alisema kila mwananchi ana wajibu wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika maeneo yake ili kuondokana na ukataji wa miti ovyo.

Alisema ukataji miti ovyo unasababisha kutokea kwa mabadiliko ya hali ya hewa, ongezeko la joto na uzalishaji wa hewa chafu.

Christopher, alitaka uhamasishaji uwafikie wananchi waishio vijijini ili waachane na matumizi ya nishati chafu kwa ajili ya kupikia majumbani kwa kuwa pia unahatarisha afya zao kwa kuvuta hewa chafu.

Alisema kwa sasa ajenda ya kitaifa ni kuhama katika matumizi ya nishati chafu kwenda nishati safi.

Alisema ni wakati wa wadau kuchangamkia fursa ya usambazaji wa nishati safi vijijini ili kuwafikia wananchi wengi na kuisaidia serikali kutekeleza mpango wake wa kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema katika kufikia azma hiyo, baadhi ya wabunge nchini wamegawa majiko na mitungi ya gesi bure kwa wananchi.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni wananchi kuelimishwa inakopatikana nishati hiyo baada ya kwisha kwenye mitungi.

Baadhi ya wadau hao akiwamo, Deus Masasi, aliiomba serikali kukarabati miundombinu ya barabara maeneo ya vijijini ili kuwarahisishia kufikisha huduma hiyo bila kikwazo.

Mwajuma Abdallah, aliwaomba wadau wa nishati safi kufungua maduka zaidi vijijini ili kuboresha huduma kwa wananchi kwa kubadilisha mitungi iliyokwisha gesi na kupewa iliyojazwa nishati hiyo.

Nipashe
TESA
Jumanne Januari 7, 2025
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

'Kwa kuhifadhi misitu, uoto asilia tutaondoa maporomoko udongo'



Ukurasa 12

KUTUNZA UBONGO (2)
Usikae gizani, acha upweke lakini chunga kompyuta, simu na runinga



Ukurasa 13

**BAYOTEKNOLOJIA**
**Kinga mabadiliko tabianchi, mbegu bora, kilimo kisicho na kemikali**

NA MWANDISHI WETU

# Virusi tishio kuliko UVIKO-19 vyadaiwa kuitikisa China tena, yapuuza madai

HABARI mbaya mwaka mpya wa 2025, ni hizi unadaiwa umekaribishwa na maradhi yanayotokana na virusi vikali kuliko UVIKO 19.

Ni mlipuko mpya wa virusi nchini China vikipewa jina la 'human metapneumovirus' (HMPV) na sasa kikubwa ni kujua dalili, vidokezo vya kuzuia na namna ya kujitibu.

Watoto wadogo, watu wazima, wazee na wale walio na kinga dhaifu kutokana na magonjwa yasiyoambukiza, wako katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa huo wa HMPV.

Kwa mujibu wa Mtandao wa NDTV wa India, ripoti na taarifa za kuwapo maradhi hayo zimesambaa kwenye mitandao ya kijamii, zikisema hospitali zimejaa watu walioambukizwa na maeneo ya kuchomea maiti yamezidiwa kutokana na vifo vingi.

Taarifa zinasema India pia inafanya uchunguzi wa kuwapo kwa maradhi hayo na imeshauri raia kuchukua tahadhari.

Baadhi ya watumiaji wa mitandao ya kijamii wanadai kwamba virusi vingi, ikiwa ni pamoja na mafua HMPV, mycoplasma pneumoniae na COVID-19, vinazunguka nchini China.

Mtandao wa gazeti la Independent la Marekani unamnukuu Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China Mao Ning, akisema : "Maambukizi ya mfumo wa kupumua huwa yanaongezeka wakati wa msimu wa baridi."

Anaongeza kuwa: "Magonjwa yanaonekana kuwa mabaya zaidi na yanaenea kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita," anasema, licha ya kwamba kuna madai kwamba China imetangaza hali ya hatari hasa eneo la kaskazini ambako maradhi hayo yanatikisa.



Matabibu katika harakati za kupambana na magonjwa ya virusi. **PICHA: MTANDAO**

HMPV husababisha dalili zinazofanana na mafua. Kwa kawaida virusi huathiri mfumo wa juu wa upumuaji ambao ni pua, mdomo, koromeo na koo na 'larynx' au kisanduku cha sauti, hivyo sauti hukwama.

Lakini wakati mwingine huweza kusababisha maambukizo ya njia ya chini ya upumuaji kwenye sehemu ya mfumo wa kupumua ambayo ni pamoja 'koromeo au trakea, pia ni njia kubwa za kupeleka hewa kwenye mapafu na zile ndogo . Mishipa ya hewa ndani ya mapafu (bronchioles) na 'alveoli' ambayo ni mifuko ya hewa ndani ya mapafu inayobadilisha hewa chafu au gesi ya kaboni na kuchukua oksjeni wakati wa kupumua.

HMPV inadaiwa ni maradhi ya kawaida zaidi katika majira ya baridi na kwenye hatua za mwanzo za msimu wa machipukizi (spring).

**TAHADHARI**

Dalili za metapneumovirus ni sawa na za mafua au homa ya kawaida. Inaweza kuenezwa kutoka kwa mtu aliyeambukizwa hadi kwa wengine kupitia kukohoa, kupiga chafya au kugusana au kushika majimaji za mwili kama makamasi, mate na damu za mtu mgonjwa.

Baadhi ya dalili za kawaida ni pamoja na kikohozi homa kali, kuziba au kubanwa pua, maumivu makali kooni, kushindwa kupumua na kukosa hewa.

Ugonjwa hulipuka baada ya siku tatu hadi sita baada ya maambukizi kutegemea ukali wa virusi na uimara wa kinga ya mwili.

**JITAMBUE**

Ni nani aliye katika hatari kubwa zaidi? Jibu ni watoto wadogo, watu wazima, wazee na wale walio na udhaifu unaodhoofisha kinga . Wako katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa huo wa HMPV.

Wakati mwingine HMPV inaweza kusababisha ugonjwa mbaya ambao unalazimisha kulazwa hospitalini. Unaambatana na 'bronkaitisi', nimonia, pumu na hata maambukizi masikioni.

**KUJIKINGA**

Vidokezo vya kuzuia maambukizi ni pamoja na kunawa mikono kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20 ili kudhibiti kuenea.

Kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa au kupiga chafya, kutumia au kuvaa barakoa na kuepuka kushirikiana au kuchangamana na wale ambao ni wagonjwa .

Kuacha kugusa macho, pua na mdomo kwa mikono ambayo haijaoshwa na kufanya mazoezi lakini pia kujitenga au kujiweka

INAENDELEA UK. 12

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

KUTUNZA UBONGO (2)

# Usikae gizani, acha upweke lakini chunga kompyuta, simu na runinga



Kutumia vipaza sauti vinavyobana kichwa na masikio huathiri usikivu na afya ubongo. **PICHA: MANDAO.**

MWAKA mpya unapoanza tahadhari za kiafya ni muhimu kuzizingatia na kufahamu cha kufanya ili kujiepusha na magonjwa mbalimbali mojawapo ni tatizo la sasa la afya ya akili.

Wapo wengi wenye changamoto hiyo na mwanzo wa mambo hayo ni matokeo ya athari mbaya kwenye ubongo. Kumbuka kulinda ubongo na kuutunza. BBC inajadili tabia 11 zinaharibu ubongo wako na jinsi ya kuzishinda.

Wiki iliyopita tulizitaja baadhi ya tabia hizo kuwa ni pamoja na kukosa usingizi, kifungua kinywa, kutokunywa maji na kuendekeza msongo wa mawazo.

Leo tunakamilisha ripoti hii kwa kuangalia mienendo ya kila siku inayoumiza ubongo.

**KUTUMIA FONI**

Vipaza sauti au foni zinazobanwa kichwani au masikioni vina madhara. Wataalamu wanasema kuendelea kutumia vinakudhuru ndani ya dakika 30.

Aidha, kusikiliza kwa sauti kubwa au kwa muda mrefu inamaanisha kelele kubwa hizo zinasababisha kupoteza usikivu.

Pia inahofiwa kwamba kusikia kwako kunapoharibika, hakuwezi kurekebishwa kikamilifu kumbuka kupoteza kusikia huathiri moja kwa moja ubongo.

Kulingana na watafiti wa Marekani, watu wenye upotevu wa kusikia au usikivu hafifu wanakabiliwa na uharibifu wa tishu za ubongo.

Hali hii huongeza hatari ya kupata shida ya kupoteza kumbukumbu na matokeo yake, inakuwa vigumu kusoma na kuzingatia, inasema BBC

Fikiria mara mbili kabla ya kutumia vipaza sauti vya masikioni au kusikiliza wimbo unaoupenda kwa sauti ya juu.

Ikiwa unasikiliza nyimbo kwa kutumia vifaa hivyo au foni masikioni kwa muda mrefu, usiongeze sauti zaidi ya asilimia 60. Pia pumzika kwa saa moja na acha kuvitumia mfululizo.

**USIPENDE UPWEKE**

Kuwa peke yako kila wakati, kutochangamana na watu, kuzungumza na kupiga hadithi si jambo jema.

Ni muhimu sana kwa afya ya ubongo wako kuzungumza na kuchangamana na watu popote, na kutumia muda mwingi peke yako ni vibaya kwa ubongo wako kama vile kutopata usingizi wa kutosha.

Kuwa na marafiki na kufurahi na familia huiweka akili za binadamu kwenye hali bora kiafya.

Ni kinyume chake kuwa mpweke kwani huongeza hatari ya unyogovu, wasiwasi na shida ya akili.

Ikiwa unataka kuweka ubongo wako kwenye afya, tumia wakati au muda mwingine na marafiki wa karibu na familia mara kwa mara. Ni vyema kuwa na watu wenye mawazo chanya'.

**HISIA/MAWAZO HASI**

Ikiwa una tabia ya kuwaza fikira hasi au mbaya kila wakati ni kuharibu ubongo. Kwa mfano kuwaza kuwa hakuna kitu kizuri kwako, wala hakiwezi kutokea, unaona dunia ni mbaya sana au huna tumaini kuwa siku zijazo ni giza si jambo jema.

Lakini pia kudhani kuwa huna bahati, ni hatari kwa ubongo. Kwa sababu mawazo mabaya huunda msongo wa mawazo, unyogovu na wasiwasi kwa upande mwingine.

Vile vile, zipo kemikali na vichocheo hujilimbikiza kwenye ubongo ambayo ni sababu kuu ya shida ya akili na kukosa kumbukumbu.

Kwa hiyo, jaribu kuacha mawazo mabaya mara moja. Kufanya hivi mara kwa mara itakuwa tabia inayokuwa na ikiwa huwezi kufanya hivyo peke yako, tafuta msaada wa daktari wa akili.

**EPUKA MABAYA**

Ili kuwa na ubongo wenye siha kuepuka urafiki mbaya pia ni muhimu sana. Mbali na hilo ni vizuri kujizuia kutazama habari mbaya za vifo, ajali, vurugu mauaji na kupenda sehemu zenye kelele na vurumai.

**KWEPA GIZA**

Ni hatari kutumia muda mwingi gizani, utafiti nchini Marekani umeonesha kuwa watu ambao hutumia muda mwingi gizani au kutumia muda mrefu katika maeneo yaliyofungwa ambapo hakuna mwanga mwingi na mzunguko wa hewa, mazingira huweka shinikizo sana kwenye ubongo.

Kwa sababu mambo yatokanayo na mwanga wa jua ni muhimu sana kwa ubongo wa binadamu. Vinginevyo, shida kama vile unyogovu zinaweza kutokea iwapo utaishi gizani..

Ili kuweka ubongo wako katika hali ya afya njema, unapaswa kwenda juani kila siku. Nenda nje. Ikiwa uko nyumbani, fungua milango na madirisha.

Pamoja na hayo kupenda kula kupindukia ni hatari kwa ubongo.

Haijalishi jinsi chakula ni 'cha afya' kiasi gani, kula kupita kiasi kunaweza kuharibu ubongo.

Utafiti umeonesha kuwa ulaji kupita kiasi pia huziba mishipa ya ubongo na kupunguza mtiririko wa damu.

Hii inasababisha kupoteza kumbukumbu na kufikiri. Ambayo inaweza kusababisha shida ya akili. Kula vyakula visivyofaa, vyakula vya kukaanga, vyenye sukari nyingi, vinywaji baridi kutokunywa maji kuna hatari kwa ubongo.

Ndiyo maana ni muhimu sana kuwa na chakula cha wastani na sahihi.

Watu wengi hutumia programu tofauti kufuatilia kalori zao za kila siku. Lakini suluhisho bora ni kutengeneza lishe yako mwenyewe kulingana na ushauri wa mtaalamu wa lishe na uifuate.

Watu wengi wanafikiria kuwa lishe ni juu ya kuondoa mafuta. Lakini kumbuka kwamba asilimia 60 ya ubongo ni mafuta. Kwa hivyo kila aina ya chakula kinapaswa kuliwa.

Lakini inapaswa kuliwa kwa kiasi kinachofaa.

Mbali na hayo, unywaji pombe na uvutaji sigara ni hatari kwa afya. Athari yake mbaya zaidi iko kwenye ubongo.

Mambo haya yanabana mishipa ya fahamu ya ubongo na kuharibu seli.

Kwa hiyo, eneo la ubongo wetu, ambapo kumbukumbu huhifadhiwa, haiwezi kukua.

**KOMPYUTA/TV**

Muda wa kutumia skrini au kuangalia kioo cha kompyuta au simu una athari kubwa kwa ukuaji wa ubongo. Utumiaji mwingi wa simu za mkononi kwa watoto husababisha uharibifu zaidi kwenye gamba la mbele, ambalo hutofautiana kutoka ujana hadi miaka 25.

Utafiti umeonesha kuwa watoto wanaotumia zaidi ya saa saba kwa siku mbele ya skrini wana gamba jembamba la ubongo.

Kwa sababu kuongea muda mrefu kwenye simu za mkononi kunaweza kusababisha shida kama vile maumivu ya kichwa, kuchanganyikiwa na uvimbe wa ubongo.

Kwa sababu hii, muda wa skrini ya watoto unapaswa kupunguzwa kabisa. Pia, usilale na simu karibu na mwili wako.

Weka simu kwenye begi badala ya mfukoni. Ikiwa unataka kuzungumza kwa muda mrefu, unaweza kuzungumza kupitia spika bila kushikilia simu kwenye sikio lako. Kutuma ujumbe wa maandishi ni bora kuliko kuzungumza.

***BBC***

## VIRUSI TISHIO KULIKO UVIKO-19 VYADAIWA KUITIKISA CHINA TENA, YAPUUZA MADAI

**INATOKA UK.11**

karantini ikiwa ni mgonjwa.

Hivi sasa, hakuna tiba maalum wala dawa ya kuzuia virusi au chanjo ya kukinga na HMPV.

Mtandao wa Cleveland Clinic, unaeleza kuwa Human metapneumovirus (HMPV) ni virusi ambavyo kwa kawaida husababisha dalili zinazofanana na homa na mafua.

Iwapo umeathirika unaweza kukohoa au kupumua kwa shida , kuwashwa pua na kuumwa na koo kukereketa pia. Aidha, si wakati wote wote ugonjwa au mafua yanakuwa makali.

Hata hivyo, watoto wadogo, watu wazima zaidi ya miaka 65 na watu walio na maradhi yanayoyonyong'onyeza kinga wako kwenye hatari kubwa ya ugonjwa huo mbaya.

SAYANSI

**NA MAULID MMBAGA**

BAYOTEKNOLOJIA

# Kinga mabadiliko tabianchi, mbegu bora, kilimo kisicho na kemikali

WATAFITI wa kilimo wamebainisha kuwa matumizi ya bayoteknolojia na uhandisi jeni ni muhimu zama hizi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye kilimo na uzalishaji chakula.

Bayoteknolojia ni teknolojia inayotumia elimu ya baiolojia kufanya utafiti wa aina mbalimbali kuboresha maisha na sasa imeimarishwa zaidi ikifanyakazi kwenye maabara za kisasa unaohusisha utafiti wa hali ya juu zaidi.

Wakizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, watafiti hao wanasema teknolojia hiyo ina umuhimu kwenye kuongeza tija ya kuzalisha mazao na kuwabadilisha wakulima kutoka kilimo cha kujikimu hadi cha kibiashara.

Aidha, wanashauri kuwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha madhara ya moja kwa moja kwenye uzalishaji mashambani, ni muhimu kwa sasa teknolojia mbalimbali ikiwamo ya uhandisi jeni zikapewa kipaumbele ili kupata ufumbuzi wa changamoto zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa kwenye kilimo.

Mtafiti wa bayoteknolojia ya kilimo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Dk. Aneth David anasema.

Dk. Aneth akizungumzia kuhusu bayoteknolojia anasema ni mkusanyiko wa teknolojia mbalimbali ambazo zinatumia sehemu ya viumbe hai ikiwamo vidubini au bakteria kwa ajili ya faida ya binadamu, hususani katika kuandaa mbegu ambazo zinakuwa na uwezo mkubwa wa kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Anasema mazao yanayotokana na mbegu zilizofanyiwa mabadiliko ya vinasaba kwa njia ya uhandisi jeni yanaongeza tija na kumnufaisha zaidi mkulima wakati wa mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri sekta ya kilimo na uzalishaji.

Akifafanua kuhusu bayoteknolojia anasema ni mkusanyiko wa teknolojia mbalimbali ambazo zinatumia sehemu ya viumbe hai ikiwemo nasaba ili kuongeza uhimilivu na uimara, nguvu za kukabiliana na magonjwa lakini pia kupata mazao kwa wingi.

Anasema ni kwa faida ya binadamu, hususani katika kuandaa mbegu ambazo zinakuwa na uwezo mkubwa wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Aneth, anasema utaratibu wa



Mtafiti wa bayoteknolojia ya kilimo UDSM, Dk. Aneth David, akiwa katika majukwaa ya mijadala ya kisayansi. **PICHA: MAULID MMBAGA**

utafiti na kuruhusu mbegu zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki kwa ajili ya chakula unahusisha majaribio ya usalama wa chakula pamoja na kupima virutubishi.

Bingwa huyo wa bayoteknoloji ya kilimo anasema mazao yanayotokana na mbegu zilizoboreshwa kwa njia ya kijenetiki yana nafasi kubwa ya kutatua changamoto za upatikanaji wa chakula salama na cha kutosha, jambo ambalo ni changamoto katika mataifa mbalimbali ya Afrika hasa kipindi cha ukame unaotokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Bayoteknolojia inatumika kutengeneza mbegu kwa ajili ya kutatua changamoto ambazo ni ngumu kutatulika kwa kutumia mbegu za asili. Mfano, magonjwa, wadudu wapya vamizi wasio na suluhisho na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame na ukosefu wa virutubishi kwenye chakula, hayawezi kutatuliwa na mbegu za asili," anafafanua Dk. Aneth.

**UMUHIMU WAKE**

Bingwa huyo anasema kwa kutumia sayansi ya kuboresha mbegu kijenetiki wanaweza kutengeneza mbegu na mazao yanayoweza kustahimili ukame, kuhimili magonjwa yasiyo na tiba kama ugonjwa wa michirizi ya kahawia kwenye mohogo yanayoweza kukua kwenye udongo usiofaa kwa kilimo cha kawaida ikiwamo wenye kiasi kikubwa cha chumvi.

Pia, anasisitiza kuwa teknolojia ya mbegu za kisasa inasaidia kuwa na mazao yanayoweza kupambana na wadudu waharibifu kama viwavi jeshi vamizi bila kutumia kemikali. Na kwamba mahitaji ya chakula yanazidi kuongezeka kutokana na kuwapo idadi ya watu lakini pia uzalishaji ukiathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Anaeleza kuwa kutokana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo ni tatizo kubwa kwenye kilimo Tanzania na Afrika, mbegu zilizoboreshwa kwa njia ya kijenetiki zinaweza kutoa suluhisho bora zaidi na la uhakika.

Akijibu suala la mbegu gani ipewe kipaumbele, anasema uamuzi kuhusu mbegu unategemea mambo mengi na hamna jibu la jumla. Na kwamba maamuzi yanatakiwa yafanyike kwa kuzingatia hoja kwa hoja kutegemea na mahitaji ya wakati, mahali na malengo.

Dk. Aneth anashauri kuwa ni muhimu kwa serikali na wadau wengine wa kilimo kuweka kipaumbele zaidi kwenye teknolojia mbalimbali zinazolenga kuleta suluhisho la kudumu kwenye ulinzi wa chakula na kilimo, ikiwamo bioteknolojia.

Anasema jamii ina nafasi kubwa ya kushirikiana na wataalamu na serikali katika kutatua changamoto za kilimo na uzalishaji wa chakula. Ila jukumu kubwa zaidi ni kwa watunga sera na inawekeza rasilimali kwenye tafiti za kilimo na maendeleo ya mbegu na kuhakikisha usalama wa chakula.

"Kama nchi hatuwezi kubaki nyuma, ni muhimu kujijengea uwezo wa kutafiti na kufikishia walaji mbegu zilizoboreshwa kwa teknolojia za kisasa kama bioteknolojia ya uhandisi jeni ili kufanikisha ututuzi wa changamoto za kilimo na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao," anasema Dk. Aneth.

**INAZUIA UHARIBIFU**

Anasema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ni muhimu kuipa kipaumbele bayoteknolojia katika kuendeleza kilimo kwasababu inasaidia mimea kujilinda yenyewe dhidi wa magonjwa na wadudu vamizi waharibifu.

Anafafanua kuwa inatumika kuandaa au kutengeneza vinasaba vinavyotumika kusaidia mmea kupambana na magonjwa mbalimbali ya moja kwa moja, pamoja na kuchanganya vinasaba vya mimea zaidi ya mmoja ila kutoa mazao bora.

"Kwenye kilimo tunatumia teknolojia hii kutengeneza mbolea hai (organic fertilizers) na katika utafiti, tumeona tunaweza kuchukua vidubini au bakteria wanaoweza kuchukua hewa ya nitrojeni wakaitengeneza ili kutumiwa na mimea.

"Kwahiyo badala ya kutumia mbolea ya kemikali ambazo zina madhara, tunatumia bakteria wanaosimama kama mbolea mbadala na kuwezesha mimea kufyonza madini kama salfa na salfeti kutoka kwenye udongo kuupa mmea nguvu na uimara," anasema Dk. Aneth.

**SULUHU YA UHAKIKA**

Meneja wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Mikocheni Dar es Salaam, Dk. Fred Tairo, anasema kuna umuhimu mkubwa wa kutumia bioteknolojia kwenye kilimo kwa sababu inawawezesha wakulima kupata mbegu zenye ufanisi na kutatua kwa haraka changamoto zinazowakabili.

Vilevile, anasema teknolojia hiyo na njia mbalimbali za kiasili inawezesha kupata dawa za haraka hasa katika kukabili magonjwa mapya yanayoibuka na kupata urahisi wa kutambua mdudu wa aina gani anashambulia mazao ya chakula na kumkabili asilete madhara.

"Kwa kutumia bayoteknolojia na matokeo ya kiutafiti tunampatia mkulima suluhu ya haraka, na teknolojia hii ina sifa nzuri kwenye mimea mfano migomba na mahindi inachochea kuongeza ufanisi.

"Teknolojia hiyo pia inatusaidia kuboresha mbegu kutoka kwenye mimea mingine, kwa ujumla ukitumia bayoteknolojia inatupa mwongozo wa kutatua matatizo yanayowakabili wakulima kwa ufanisi na haraka," anasema Dk. Tairo.

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# ‘Kwa kuhifadhi misitu, uoto asilia tutaondoa maporomoko udongo’

WATANZANIA wanaendelea kufurahia mwaka mpya 2025, wakisubiri mvua za masika, lakini pia kutafakari vifo na hasara zinazotokana na maporomoko ya udongo kila mwisho wa mwaka.

Itakumbukwa kuporomoka kwa udongo Katesh wilayani Hanang yalitokea Desemba 2023 na mwaka huu kumeripotiwa mengine Same mkoani Kilimanjaro.

Maporomoko hayo ni matokeo ya matumizi mabaya ya ardhi, yasiyoendelevu yanayosababisha misitu na uoto wa asili kutoweka kwa kasi na kuhatarisha maisha ya binadamu na viumbehai wengine.

Tanzania ni mojawapo ya nchi zenye misitu na uotoasilia kwa asilimia kubwa, wakati wa uhuru karibu miaka 64 iliyopita, sehemu kubwa ilikuwa imefunikwa na misitu asili.

Lakini taarifa iliyotolewa 2015 na Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia mradi wa kupima na kutathmini, misitu ilionyesha kuwa eneo lenye misitu Bara ni hekta milioni 48.1 (sawa na asilimia 55 ya eneo lote).

Misitu aina ya “miombo” imetapakaa maeneo mengi nchini hususan kwenye ardhi inayomilikiwa na vijiji. Upande mwingine, kuna misitu inayofunika milima mathalan, Kilimanjaro na Meru, Livingstone na Rungwe kadhalika misitu katika hifadhi za taifa kama Ngorongoro, Uduzungwa pia mikoani Kagera, Katavi, Kigoma, Rukwa pamoja na baadhi ya maeneo kwenye mapori ya akiba.

Ingawa takwimu zinaonyesha Tanzania Bara imefunikwa na hekta milioni 48 za misitu, kiuhalisia misitu imetoweka kwa kiwango kikubwa.

Kwa miongo minne iliyopita, kasi ya kukata miti, kufyeka misitu ya asili imekuwa ikiongezeka. Hadi sasa zaidi ya hekta 400,000 zinatoweka kila mwaka.

Kisa ni ongezeko la watu kutoka chini ya milioni 10 mwaka 1961 na zaidi ya milioni 60, wanapoongezeka, mahitaji ya maeneo ya kuishi, kilimo na mifugo vinaongezeka pia.

Kadhalika, kumekuwapo vijiji vingi zaidi ya 12,000, pia miji na majiji hupanuka wakati huduma za mipangomiji zikibaki nyuma.

Hivyo, kusababisha baadhi ya misitu ya asili kumezwa.

Halikadhalika, mahitaji ya mazao ya misitu mathalani mbao, nguzo, mkaa na kuni yakaongezeka kasi yake ikichochea



Waokoaji wakitafuta miili kwenye matope ya mafuriko na maporomoko ya udongo Hanang Desemba 2023. **PICHA: MTANDAO**

ukataji miti.

Ukiyajumlisha hayo pamoja na athari zinazotokana na kilimo cha kuhamahama, kuchoma mapori moto, kiangazi pamoja na misitu ya asili kutotunzwa au kutosimamiwa ipasavyo matokeo hasi yameendelea kuongezeka.

Yamesababisha sehemu nyingi kupoteza uotoasili (natural vegetation cover) hivyo ardhi kuathirika kwa kiasi kikubwa kwa vile haifunikwi na nyasi, majani, mimea, miti na misitu.

Shughuli nyingi za kibinadamu zinapoongezeka bila kujali uwepo na umuhimu wa uotoasili kwa ajili ya kuhifadhi ardhi na udongo kutunza mazingira, wanaoathirika zaidi ni binadamu na viumbehai wengine.

Kiikolojia, misitu pamoja na uoto asilia nyasi na majani, mimea kwenye mbuga au maeneo mengine husaidia, kwa kiasi kikubwa, kufunika ardhi au udongo ili kuzuia mmomonyoko kutokana na kasi kubwa ya upepo mkali au maji ya mvua.

**KUPOROMOKA UDONGO**

Maafa yanayojitokeza Tanzania mfano, kuporomoka ardhi au udongo huko Hanang, mkoani Manyara mwaka juzi na kuharibu eneo la mji mdogo Katesh na viunga vyake mathalani, Gendabi yalisababishwa na mvua kubwa.

Ikumbukwe yalikuwa maporomoko makubwa ambayo hayajawahi kutokea kwenye eneo la Mlima Hanang na kusababisha, bila kutarajia, mafuriko ya mawe, magogo na maji mengi yakitiririka kutoka milimani.

Hali hiyo, ilizua taharuki na sintofahamu kwa wakazi wa maeneo ya Katesh, maporomoko hayo yakiharibu nyumba za wananchi zaidi ya 100 na baadhi ya watu kupoteza uhai.

Serikali ikalazimika kutumia fedha nyingi kuwasaidia wananchi walioathirika kwa kuwajengea nyumba na kurejesha huduma muhimu za kijamii.

Kadhalika, mwezi uliopita wilayani Same, mkoa wa Kilimanjaro, yalitokea maporomoko ya ardhi na udongo kutokana na ardhi kukosa uotoasili na misitu ya kuhifadhi udongo ili ubaki mahali pake. Kiikolojia miti na uoto mwingine wa asili ni mhimili wa kuhifadhi eneo kutokana na mizizi yake kuushikilia udongo.

Kadhalika, misitu au miti husaidia kupunguza kasi au nguvu ya maji au mvua hivyo kuwezesha maji ya mvua kuingia ardhini taratibu bila kuleta madhara.

Sehemu zenye upepo mkali pia misitu na miti hudhibiti kasi na nguvu ya upepo huo mkali, na kuzuia chembechembe za udongo kupeperushwa kupelekwa mbali.

Uharibifu unakuwa mkubwa kwenye sehemu zenye miinuko na milima hasa maeneo ambayo uotoasilia hakuna na misitu imeharibiwa kiasi cha kuiacha ardhi tupu bila kufunikwa.

Kumekuwepo mazoea ya kulima kwenye miteremko mikali bila kuchukua tahadhari ili kuzuia mmomonyoko na maporomoko ya ardhi na udongo hasa inapotokea mvua kubwa.

Maafa yaliyotokea Katesh na Same kisababishi kikubwa ni udongo milimani kubaki bila kufunikwa na misitu au uotoasilia hivyo kukosa cha kuushikilia.

Mvua kubwa ziliponyesha maji yakawa mengi ardhini na udongo ukalegea hivyo kupelekea maporomoko makubwa yenye udongo, mawe, miti, na vingine vingi kutoka milimani kwenda yalipo makazi ya watu hadi kusabatisha hasara kubwa.

Mathalani, hali ilivyotokea wilayani Same ikiwamo watu sita kupoteza maisha na nyumba 25 kubomolewa hivyo kuacha wengi hawana pakuishi.

Itakumbukwa mwaka 1963 kulitokea maafa katika eneo la Shume-Manolo wilayani Lushoto baad[illegible]aziri wa Ardhi, wakati huo kuwaruhusu wananchi walime kwenye sehemu zenye miteremko mikali.

Asimwe Novath.

Kitendo cha kuifyeka misitu na kupanda mahindi hakikuwaacha salama. Iliponyesha mvua kubwa kukatokea maporomoko makubwa ya udongo, mawe makubwa na takangumu nyingine vikafunika makazi ya watu.

Ruhusa ya kulima ilitolewa kisiasa lakini kitaaluma na kiikolojia hayakuwa maamuzi sahihi, japo yalijiri kwa nia njema ya serikali kuwasaidia wananchi lakini matokeo yakawa kilio kikubwa. Tokea hapo serikali ikakataza watu kulima kwenye miteremko ya milima.

Kwa kuwa binadamu husahau tukio hilo lilifutika kwenye kumbukumbu za walioshuhudia ajali hiyo mbaya sababu ya kufyekwa misitu kwenye milima hatarishi ili kupata chakula ambacho hakikupatikana badala yake kukatokea kuporomoka ardhi.

Pamoja na watu kuwa wengi na mahitaji ya chakula kuongezeka, ufyekaji misitu umekithiri hadi kulima kwenye milima, miteremko hatarishi na vyanzo vya maji.

Viongozi serikalini, nje ya serikali na wadau tambueni kwamba rasilimali misitu, uotoasilia kwenye milima na miterenko mikali ni muhimu sana hivyo itunzwe kwa nguvu zote.

Sera za uhifadhi na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, vitekelezwe kivitendo na usimamizi wa sheria uimarishwe.

Tukisema sehemu fulani binadamu asiingie kulima, wala kuazisha makazi, kufyeka misitu na kukata miti au kuchunga, kufuga mifuko, iwe hivyo. Vijiji viweke sheria za kuhakikisha maeneo yenye milima, miteremko na ardhioevu kama vyanzo vya maji, yatambulike vijijini na kuyahifadhi ipasavyo. Tusisubiri maafa yatokee, kuzua taharuki halafu ndipo tuchukue hatua: kumbuka kinga ni bora kuliko tiba, tulitambue hili na tulisimamie bila kuoneana haya hasa ndugu na jamaa kwa kufanya shughuli za kibinadamu sehemu hatarishi zitakazopelekea taifa kupatwa na maafa kutokana na maporomoko ya ardhi na/au mmomonyoko wa udongo.

Matukio kama hayo yakiendelea kutokea itadhihirisha wengi wetu kukosa maarifa stahiki na kushindwa kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni husika.

Sheria ya kutunza, kulinda na kusimamia mazingira nchini iweke mkazo kwenye kutunza na kuyasimalia maeneo yote nyeti na kuhakikisha yasiharibiwe na binadamu kwa maslahi binafsi, bali yatunzwe kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

Tumerithi nasi tuwarithishe.

Hii ni pamoja na kuhakikisha misitu na uotoasilia kwenye maeneo hatarishi, havifyekwi wala kuchomwa moto ovyo. Sheria kali ziwekwe na watakaothibitika kufanya vitendo vya kuhatarisha mazingira kwa faida binafsi wadhibiwe vikali maana hao ni wahujumumazingira kiasi cha kusababisha binadamu kupoteza maisha au kuumizwa vibaya na maporomoko ya ardhi na udongo yanapotokea.



HABARI DODOMA

## Meya atamani vijiwe vya bao kuchochea maendeleo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MSTAHIKI Meya wa Manispaa ya Singida, Yaghi Kiaratu ametaka vijiwe vya mchezo wa bao vya wazee kutoa ushauri kuleta maendeleo ya Singida kwa manufaa ya wananchi na taifa.

Kiaratu alitoa hauli hiyo wakati akizungumza na wanachama wa kikundi cha Amani katika hafla ya kuwapa zawadi washindi watatu.

"Mchezo huu wa bao waasisi wetu wa taifa wakati wanatafuta uhuru waliutumia kuzungumzia siri za uhuru hivyo na sisi tutumie bao ili kuijenga Singida yetu kwa maendeleo na sio majungu," alisema.

Kiaratu, alisema kwa kuwa mchezo huo unapendwa zaidi na wazee, ushauri watakaoutoa kwa vijana utasaidia kudumisha maadili na amani katika mji wa Singida.

Alisema Amani kikisajiliwa na kutambulika kisheria, kitatumika kama fursa ya kupata mikopo kwenye taasisi za fedha.

"Sisi mjini hatuna mashamba, mashamba yetu ni kujishughulisha na kazi mbalimbali, huyu atauza mtumba, yule kuku, ndio mashamba yetu. Kikundi hiki mtaenda kwenye mchezo wa kuwekeza na mkawa mnapeana mitaji, hivyo mkainuana kiuchumi," alisema.

Alisema kwa kupata kazi za kunawaepusha kujiingiza katika mambo mabaya si tu kwa vijana, pia wazee.

"Kundi lenu hili ni muunganiko wa watu wengi ambao wametoka maeneo mbalimbali katika Manispaa ya Singida, kwa hiyo ni lazima litambulike kwa kulisajili na mimi naahidi nitalipia gharama zote za usajili ili ikitokea fursa mnapata mikopo kupitia kikundi," alisema.

Mratibu wa Kikundi cha Amani, Dk. Philip Kitundu, alimwomba Meya huyo kuwasaidia ili kiweze kupata mkopo halmashauri na kusajiliwa.

"Amani kina wajasiriamali, wafanyabiashara ndogo ndogo na kwa kutumia biashara zetu tukipata mkopo tutaweza kujiongezea kipato na tupo tayari kurejesha fedha hizo kwa wakati kwa kuzingatia masharti ya mkopo," alisema Dk. Kitundu.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Mufumbu wilayani Singida, Amani Songaraeli, akitoa maelezo kwa Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima (mwenye suti nyeusi), jana baada ya kutembelea ujenzi wa madarasa na mabweni ya kidato cha tano katika shule hiyo. Mbunge huyo alitoa wito kukamilishwa ujenzi huo haraka. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mirembe yavunja ukimya, yatibu magonjwa yote

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JAMII imetakiwa kuachana na imani potofu kuwa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ni mahususi kwa ajili ya wagonjwa wa vichaa na kujitokeza kupata matibabu ya magonjwa mbalimbali.

Dk. Godfrey Mkama, daktari katika hospitali hiyo alitoa wito huo juzi baada ya Klabu za Dodoma Jogging kushiriki mazoezi na kufanya usafi kwa lengo la kuhamasisha jamii kushiriki mazoezi ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza.

"Serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imefanya uwekezaji mkubwa kwa kutupa vifaa tiba vya kisasa na kuboresha miundombinu na kuongeza wataalamu ili wananchi wapate huduma bora za afya na uwekezaji uweze kuleta tija kwa jamii," alisema Dk. Mkama.

Alisema licha ya hospitali hiyo kuhudumia watu wanaokabiliwa na matatizo ya afya ya akili, msongo wa mawazo, uraibu wa pombe, bangi na vilevi vingine, wananchi wanapaswa kuitumia kupata matibabu ya magonjwa mengine.

Alisema kutokana na uwepo wa madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake, watoto, macho na mifupa ni nafuu kuliko hospitali nyingine nchini kwa kutumia bima na malipo taslimu.

"Mkaribie sana hapa kuna vitengo vya wataalamu wa saikolojia, usisubiri uumwe, ukiangalia hivi sasa maisha yetu tunakimbizana, kitu kidogo utahitaji ushauri. Mfike hapa watawahudumia kwa ufanisi," alisema Dk. Mkama.

Mkurugenzi wa Huduma Saidizi wa Hospitali hiyo, Bakar Abdulrahman, alitoa rai kwa wananchi kulinda afya zao kwa kupunguza matumizi ya wanga, sukari, kufanya mazoezi na kuzingatia mtindo bora wa maisha ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.

"Nawashukuru wanamichezo wote kwa mazoezi mazuri kwa ajili ya afya zetu kwani kufanya mazoezi mara kwa mara inasaidia kuboresha afya ya mwili na akili," alisema.

Mwanachama wa Klabu ya Dodoma Fitness, Zamoyoni Komba, alitoa wito kwa wataalamu wa lishe kushirikiana na wanamichezo kutoa elimu ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kwa jamii.

Aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kujiunga na vikundi vya mazoezi ili kulinda afya zao na kundokana na magonjwa hayo yasiyo ya kuambukizwa kama sukari na shinikizo la damu.

# Mtoto atoweka nyumbani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA



MTOTO wa kike, Paulina Naronyo (11), Mkazi wa Kata ya Hazina jijini hapa, ametoweka nyumbani kwao zaidi ya wiki tatu na hadi sasa hajulikani alipo.

Mama mlezi wake, Esupat Saringe, akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake jana, alisema mtoto huyo (pichani) alitoweka nyumbani kwao hapo katika mazingira ya kutatanisha tangu Desemba 16, mwaka jana na hadi sasa hawajafanikiwa kumpata.

"Mtoto huyo aliondoka akiwa amevaa gauni ya maua ya njano na kijani hadi leo hatujampata. Alitoka nikiwa ndani, nikajua atarudi lakini hadi sasa hatujui alipo," alisema na kuongeza kuwa:

"Tulitoa taarifa Kituo cha Polisi na kupatiwa RB namba DOM/RB/17400/2024. Pia tumezunguka kwenye makanisa, misikitini, mikusanyiko ya watu, kutoa matangazo na kubandika picha yake maeneo mbalimbali bila ya mafanikio."

**Aliwaomba wasamalia watakaomuona mtoto huyo watoe taarifa kituo chochote cha Polisi au wapige simu namba 0695570079 na 0788545207.**

# Askofu 'awakanya' vijana udukuzi mitandaoni

**Na Renatha Msungu** DODOMA

ASKOFU Msaidizi wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo wa Msalaba Jimbo Kuu la Dodoma, Wilbroad Kibozi, amewataka vijana kutumia elimu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuleta maendeleo ya taifa na si udukuzi kwenye mitandao.

Askofu Kibozi alitoa rai hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Epifania na sherehe za ukaribisho wake zilizofanyika juzi katika kanisa hilo lililopo jijini hapa.

Alisema baadhi ya vijana wanaitumia vibaya taaluma hiyo kufanya uhalifu, kitendo ambacho hakikubaliki kwenye jamii.

Alisema kupitia maadhimisho hayo na mwaka huu wa Jubilei wanapaswa kubadilika.

"Hayo ni matumizi mabaya ya vipaji ambavyo mmepewa na Mungu, mnapaswa kuvitumia kufanya mambo mema ambayo yanaleta maendeleo kwa jamii ya kumpendeza Mungu," alisema Askofu Kibozi.

Alisema wanapaswa kubadilika ili kuondoa hofu ndani ya jamii kuhusu matumizi mabaya ya mitandao na kutumia utaalamu kuelimisha.

"Naomba mbadilike watu wanakosa amani na simu zao za mkononi kwa sababu ya udukuzi wa taarifa za mitandaoni na kuzitumia vibaya," alisema Askofu huyo.

Alisema taaluma hiyo ya teknolojia ya mawasiliano ni bora na inakubalika duniani kote, hivyo vijana wanapaswa kuitumia kwa mambo mema ya kumpendeza Mungu na jamii.

Aliwakumbusha waumini kujenga utaratibu wa kusaidiana katika masuala ya msingi, kukumbuka kusaidia watu wasiojiweza kwa kutoa misaada ili nao wajione kama sehemu ya jamii.

Kobizi, alisema wanapaswa kujenga utaratibu wa kufundisha upendo katika familia ili kusaidia kuwatengeneza watoto katika misingi bora tokea wakiwa wadogo na baadae kuwa viongozi bora wa kiroho na serikali.

Alifafanua zaidi ya kuwa msingi mzuri wa watoto unaanzia katika malezi bora ya wazazi na walezi ambao wanakuwa nao katika maeneo mbalimbali, huku akisisitiza waumini wakumbuke kuliombea amani taifa.

Alisema wanaposali wanapaswa kuombea amani nchi, viongozi wa dini na serikali ili kutekeleza wajibu wao katika misingi bora ya kiimani.



# TARI kupanda miparachichi 500 Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini hapa, inatarajia kupanda miti 500 ya miparachichi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ili kukuza uchumi wa wananchi na kutunza mazingira.

Hayo yalibainika jana wakati wafanyakazi wake walianza kupanda miti hiyo ya matunda kuzunguka maeneo ya kituo hicho kwa ajili ya kuwafundishia wakulima kilimo bora cha matunda hayo.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Dk. Denis Tippe, alisema watatumia miti hiyo kuwafundisha wakulima namna bora ya kuongeza uzalishaji na kipato miongoni mwao.

"Mparachichi ni matunda, lakini pia yanasaidia kutunza mazingira kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi, kwa hiyo hapa tutaendelea kupanda miti hii na tunawakaribisha wananchi kuja kujifunza," alisema Dk. Tippe.

Mtafiti wa Matunda wa Taasisi hiyo, Daud Mbongo, alisema miti hiyo itakayopandwa kwa mikoa hiyo ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma na Katavi itatumika kama shamba darasa ya kufundishia wananchi.

Mbogo, alisema miti hiyo wataipanda kwa kushirikiana na wadau wa kilimo, watafiti na wazalishaji wa miche ya matunda ya aina mbalimbali.

Alisema miti hiyo ya miparachichi, wanapanda kwa kuzingatia aina ya hali ya hewa ya mkoa husika na udongo.

"Tupo na wadau mbalimbali, tunafanya utafiti na kupima afya ya udongo kabla ya kuanza kupanda miti hii, wananchi watajifunza na kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa," alisema Mbongo.

Baadhi ya watafiti wa matunda na wadau wa mazingira walioshiriki kupanda miti hiyo, walisema endapo itatuzwa vizuri itasaidia kurejesha mazingira yaliyokuwa yameharibiwa.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Denis Tippe, akipanda mti wa parachichi kwenye mashamba ya kituo hicho juzi wakati wa uzinduzi wa upandaji wa miche 500 ya maparachichi kwa ajili ya kufundishia wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanakijiji kicheko maji ya uhakika

**Na Mwandishi Wetu,** CHUNYA

WAKAZI wa Kijiji cha Soweto kilichopo Kata ya Kasanga wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji baada ya serikali kukamilika mradi wa kisima.

Mradi huo umetekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na Shirika lisilokuwa la kiserikali la CRS kwa lengo la kutatua kero ya maji katika kijiji hicho.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wakazi hao, walisema kabla ya mradi huo kukamilika, walikuwa wanahangaika kupata huduma hiyo hasa kipindi cha kiangazi kutokana na ukame.

Mmoja wa wakazi hao, Neema Sione, alisema maji waliyokuwa wanayatumia ni ya kwenye makorongo ambayo walikuwa wanachangia na wanyama na kuhatarisha afya zao.

Alisema baada ya mradi huo kukamilika, wameanza kupata huduma hiyo jirani na makazi yaona kupunguza ugomvi wa kifamilia na wenza wao.

"Tunaishukuru serikali kwa mradi huu maana sasa tunaona uhalisia wa kauli ya kumtua mama ndoo kichwani, hapa tunachota maji kwenye maeneo ya jirani sana na nyumba zetu," alisema Neema.

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Chunya, Olineno Sanga, alisema kukamilika kwa miradi ya visima kumeongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka asilimia 32 mpaka 52.

Sanga, alisema wanaendelea na utekelezaji wa miradi katika maeneo mengine wilayani hapa ili kuhakikisha wanatatua tatizo la upungufu wa maji katika wilaya hiyo.

# Mipaka vijiji Busokelo yaanza kupimwa

**Na Nebati Msokwa,** RUNGWE

TUME ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeanza kupima upya mipaka ya vijiji 14 vya kata nne za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo Mkoa wa Mbeya ili kutatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Meneja wa Tume hiyo Kanda ya Kusini, Pili Msati, alisema upimaji huo unafanyika kupitia Mradi wa Uboreshaji na Usalama wa Miliki kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kuwa na matumizi bora ya ardhi.

Alisema wananchi watakaonufaika na mradi huo wilayani Rungwe watasaidiwa kupanga matumizi ya ardhi yao na kuainisha mipaka ya maeneo yao ili kumaliza migogoro ya ardhi waliyonayo.

Maofisa watendaji wa vijiji vya Mwela na Kilasi vilivyopo Kata za Kandete na Luteba, walisema mradi huo utakuwa na manufaa kwa wananchi kwa kuanza kutumia ardhi yao kwa kuzingatia shughuli zao za kiuchumi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mwela, Pendo Mwasajile, alisema mradi huo ukikamilika utawasaidia wananchi kujua maeneo yaliyotengwa kwa kilimo, ufugaji na biashara na kuondoa migogoro miongoni mwao.

Pendo, alisema kwa sasa wananchi wanafanya shughuli zao za kiuchumi bila ya kuwapo kwa mipango ya matumizi ya ardhi na kusababisha mwingiliano na kuzaa migogoro.

"Utakuta mkulima ana shamba lake katika eneo fulani na huko huko tena mfugaji ametenga eneo lake la malisho, sasa mifugo ikivuka eneo lake na kuingia kwenye shamba la mkulima unaibuka mgogoro, mradi huu ukikamilika tunaamini migogoro ya aina hiyo haiwezi kujitokeza," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kilasi, Haimis Gasper, alisema mradi huo utawasaidia wananchi kufanya kazi zao za kiuchumi kwa kujiamini.

Alisema kupitia mradi huo anaamini migogoro ya muda mrefu baina ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo itamalizika kwa kuwa upimaji huo pia utaanisha mipaka yao na ile ya hifadhi.

Baadhi ya wananchi ambao wamefikiwa na mradi huo walisema utawasaidia kuwa na matumizi sahihi ya ardhi yao na kupata mikopo taasisi za fedha kujikwamua kiuchumi.

Mkazi wa Kijiji cha Kilasi, Benon Kiberiti, alisema anasubiri kwa hamu kumalizika mradi huo akitarajia kupata hati ya ardhi yake ambayo ataitumia kama dhamana ya kupata mikopo taasisi za fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za kiuchumi.

## Jafo akunwa maonesho Nyamanzi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Selemani Jafo amesema Serikali ya Zanzibar imelipa heshima kubwa eneo la Maonesho ya Biashara Nyamanzi Dimani kwa kukutanisha watu mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Jafo alitoa kauli hiyo wakati akifungua Maonesho ya 11 ya Biashara ya Mapinduzi ya Zanzibar katika viwanja hivyo vilivyopo Nyamanzi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha eneo hilo linakuwa kielelezo kwa upande wa biashara na kuwa kitovu nchini, Afrika Mashariki na Kati.

Jafo, alisema serikali imeendelea kufanya kazi kubwa ili eneo hilo liwe kivuto cha biashara na uwekezaji na kuinua uchumi wa wakazi wa eneo hilo.

Alisema kwa sasa biashara duniani imebadilika, hivyo maonesho hayo yatafunguwa mwanga wa biashara katika mfumo wa kidigitali.

Alieleza kufurahishwa na ubunifu wa kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchini kwa kutengeneza pikipiki zinazotumia umeme.

Aliwataka Watanzania kuwa na tabia ya kupenda biashara zinazotengenezwa nchini ili kusaidia kujenga uchumi kusonga mbele.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Fatma Mbarouk, alisema maonesho hayo yana lengo la kuwasaidia wafanyabiashara kukutana na wengine kubadilishana uzoefu na kuonesha bidhaa zao.

Alisema tangu kuanzishwa kwake mwaka 2014, washiriki wameongezeka kutoka 109 hadi kufikia zaidi 400 kwa mwaka huu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar, Ali Amour Suleiman, alisema maonesho yao yana lengo la kuimarisha biashara na kufungua fursa za uwekezaji kupitia biashara mtandaoni.

Kauli mbiu ya maonesho hayo kwa mwaka huu ni: "Biashara Mtandao kwa Maendeleo ya Biashara na Uwekezaji".

**Aliwataka Watanzania kuwa na tabia ya kupenda biashara zinazotengenezwa nchini ili kusaidia kujenga uchumi kusonga mbele.**

# ZRA yajivunia kuvuka lengo ukusanyaji mapato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA, imesema imevuka lengo kwa kusanya shilingi bilioni 75.582 kwa kipindi cha Desemba mwaka jana kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Kamishna Mkuu wa ZRA, Said Ali Mohamed wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa kuhusiana na mafanikio ambayo mamlaka hiyo imepata kwa kipindi hicho ikilinganishwa na mwaka jana.

Mohamed, alisema wamevuka ukusanyaji wa kodi kwa kipindi hicho cha mwaka jana na kuvuka lengo kwa asilimia 100.11.

Alisema mamlaka hiyo ilipanga kukusanya shilingi bilioni 75.501 kwa mwezi huo na kuvuka lengo hilo kwa kukusanya Sh. bilioni 75.582.

Akizungumzia kuhusu makusanyo Desemba mwaka juzi, alisema yalikuwa Sh. bilioni 63.513.

Alisema makusanyo hayo kwa mwaka jana, yanaonesha ongezeko la Sh. bilioni 12.069 sawa na wa asilimia 19.

Mohamed, alisema katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025, ZRA ilikadiriwa kukusanya Sh. bilioni 225.171 na kuvuka lengo kwa kupata Sh. bilioni 228.098, sawa na asilimia 101.30.

"Kwa kulinganisha na makusanyo ya robo ya pili ya mwaka uliopita wa 2023/2024, ambayo yalikuwa ni Sh. bilioni 189.937, yanaonesha ongezeko la makusanyo ya Sh. Bilioni 38.161 sawa na ukuaji wa makusanyo ya asilimia 20.09," alisema.

Alisema katika kipindi cha nusu ya kwanza cha Julai hadi Desemba jana, ZRA ilikadiriwa kukusanya sh.bilioni 419.203 na kupata sh.bilioni 429.033 ambazo ni asilimia 102.34.

Alisema Julai hadi Desemba ya mwaka wa juzi walikusanya Sh. bilioni 351.769, ikilinganishwa na ya Desemba ya mwaka 2024 yanaonesha ongezeko la makusanyo ya sh.bilioni 77.269 sawa wa asilimia 21.96.

Alisema mafanikio hayo yametokana na sababu mbalimbali, ikiwamo uwekezaji mkubwa kwenye ujenzi wa miundombinu, huduma za jamii na kuimarika kwa shughuli za uchumi Zanzibar.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (kushoto), akielekeza jambo kwa Msaidizi Mrajisi wa Mali na Ubunifu, Mustafa Abdulhamid, alipotembelea mabanda mbalimbali katika hafla ya Ufunguzi wa Maonesho ya 11 ya Biashara ya Kimataifa Dimani Magharibi B, Unguja. Ikiwa ni Shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: PIGAPICHA WETU**

# Waziri asisitiza amani idumishwe Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbaraka Mnyaa amehimiza amani na utulivu wa kisiasa kuendelea kudumishwa kwa kuchangia kuimarika sekta ya utalii na uwekezaji.

Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa hoteli ya kitalii ya Palumbo Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mnyaa, alisema kasi ya uwekezaji visiwani hapa imeongezeka katika sekta ya utalii na kuwa tegemeo kwa Zanzibar kwa asilimia 30.

Alisema hali hiyo imechangiwa na kuimarika kwa amani na utulivu na sera nzuri za uwekezaji.

Waziri huyo, alisisitiza amani hiyo inatakiwa kudumishwa kwa muda wote kwa sababu ndiyo hazina itakayosaidia kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

"Zanzibar inatajwa duniani kote ambapo sekta ya uwekezaji wa miradi mbalimbali imeshika kasi na hiyo inatokana na kudumishwa kwa amani na utulivu kwa hivyo wananchi tuidumishe kwa faida yetu," alisema.

Alimpongeza mwekezaji wa hoteli hiyo kwa kutoa ajira kwa wazawa kwa asilimia 80.

Meneja wa hoteli hiyo, Pablo Palumbo, alisemaameridhishwa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa kuimarisha sekta ya uwekezaji na kuwa kituo kimoja.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uwekezaji na Uchumi, Sharif Ali Sharif, alisema miradi ya uwekezaji katika sekta ya utalii nchini imechukua nafasi ya asilimia 37, huku 22 ni ya uwekezaji wa miradi ya nyumba.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini Unguja, Rashid Msaraka, alisema wameimarisha doria katika ukanda huo wenye idadi kubwa ya hoteli ili kudhibiti matukio ya uhalifu.

Mkurugenzi Mkuu wa ZIPA, Saleh Saada Mohamed, alisema sheria ya uwekezaji namba 10 ya mwaka 2023 imeleta mafanikio na kuondoa urasimu katika uwekezaji kwa wawekezaji nchini na kuifanya ZIPA kuwa bora Afrika ya Mashariki na Kati.

Mohamed, alisema sheria hiyo inalenga kufungua fursa zaidi za uwekezaji kwa kuongeza vivutio kwa kampuni na mashirikia kuwekeza mitaji yao nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HELEN HERIEL MATECHI** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 394715** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **08/04/2021.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/3496/2025.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**OBED M. NALSON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2223-0053** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IWAMBI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/565/2025.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**DANIEL RAYMOND MWACHA** naomba kutangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria yenye namba **TAE466255** iliyotolewa Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe 08/04/2022. imepotea tarehe 3/4/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/52713/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**DERICK MATHEW RAMADHAN,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1998-0013** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BRAINY HEROES BOYS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021, Cheti cha kuzaliwa na Laptop (Compaq). Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi, **PHQ/MOR/MOR/43021/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OSMUNDI JOHN MUKUNGILWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 188 DRJ – MITSUBISHI AERO MIDI.** Chassis namba: **MK517J20172.** Engine namba: 6D16664478. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/66/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NAFTAR M NYENZA ANATANGAZA** KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA MINI BUS** YENYE RANGI NYEUPE NA USAJILI **T805 CHR** KWA JINA LA SALIM SALEH BAGHOZAH KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/276/2025.**

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**AIDAN JERMANUS MWAGENI** anatangaza kupotelewa na Offer ya kiwanja **PLOT NA. 528 BLOCK "DD"** kilichopo Majengo Shinyanga Manispaa. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/SHI/SHI/10086/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 32258 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**VENANCE PETER MSOFE...............MAREHEMU**

**JULIUS VENANCE PETER MSOFFE..........MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 28 Mwezi JANUARI, Mwaka 2025.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe **23 Mwezi DISEMBA, 2024.**

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA KIHONDA, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...02/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ELIEZERI JOSEPH MCHOMVU wa FOLKLAND**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA UZEEL ELIEZERI MCHOMVU**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 01 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 06 mwezi 01 mwaka 2025

..............................................
**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA**
**(JENGO LA WIZARA YA ARDHI – KIVUKONI)**

**MAOMBI MADOGO NAMBA. 256/2024**
**JULIUS CHIPALA NYAMAKWELO..................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SHARIFA OTHMAN KHALID................MJIBU MOMBI NA. 1**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD.................MJIBU MAOMBI NA. 2**
**JUCACO AUCTION MARTH DEBT COLLECTOR & COURT BROKERS LIMITED..................MJIBU MAOMBI NA. 3**
**RAMADHANI JUMA FIKIRINI...................MJIBU MAOMBI NA. 4**

**<u>KUITWA SHAURINI</u>**

**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED**
**JUCACO AUCTION MARTH DEBT COLLECTOR & COURT BROKERS LIMITED**
**RAMADHANI JUMA FIKIRINI.............POPOTE MLIPO**

**JULIUS CHIPALA NYAMAKWELO** amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (Jengo la Wizara ya Ardhi – Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 22/01/2025 saa 8:00 mchana. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta kiapo kinzani "counter affidavit" ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hautatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 31 Mwezi Disemba, Mwaka 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI.......LA 20...........**

**JOSEPHINE AUGUSTINE YONAH.........MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MWITA MARWA KISBOI**

**BAKARI LITONGOLELE............MDAIWA/WADAIWA**

**<u>WITO KUITWA SHAURINI</u>**

1. **MWITA MARWA KISBOI**
2. **BAKARI LITONGOLELE**

**<u>POPOTE ULIPO/MLIPO</u>**

**JOSEPHINE AUGUSTINE YONAH** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 05/2/2025 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 Mwezi 12...2024.

MWENYEKITI

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**P.O.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail:**

**advertise@guardian.co.tz,**

**website:**

**www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARIKIMATAIFA

# Jenerali Muhoozi atishia kumuua Bobi Wine

**KAMPALA, Uganda**

MKUU wa Majeshi nchini Uganda (CDF), Jenerali Muhoozi Kainerugaba ambaye ni mtoto wa Rais Yoweri Museveni, amesema mtu pekee anayemzuia kumshughulikia mwanasiasa mkuu wa kambi ya upinzani nchini humo, Robert Kyagulanyi maarufu (Bobi Wine) ni baba yake Rais Museveni.

Jenerali Muhoozi, aliyasema hayo jana kupitia chapisho alililoliweka katika ukurasa wake wa X (zamani Twitter), akisema endapo Rais Museveni asingekuwapo angemkata kichwa Bobi Wine, akieleza kuwa hata mwanasiasa huyo mwenyewe analijua hilo.

Baada ya matamshi hayo ya Jenerali Muhoozi, Bobi Wine aliibuka na kumjibu akisema "Kitisho cha Mtoto wa Museveni ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Uganda, la kunikata kichwa sio kitu ninachokichukulia kwa wepesi hasa ukizingatia kwamba watu wengi wameuawa na yeye na baba yake na kwa kuzingatia pia majaribio kadhaa ya kuondoa uhai wangu, nakataa kutishwa na utawala wa uoga, dunia inatazama".

Wakati huo huo, Jenerali Muhoozi alisema lilikuwa ni wazo lake na majenerali wenzake kumshawishi Rais Museveni kumtumia Bobi Wine kama pandikizi la kumwondolea nguvu Kiza Besigye na kumfanya asiwe kiongozi wa upinzani mwenye nguvu Uganda.

Pia alisema baada ya kumpa pesa nyingi Bobi Wine na akapata nguvu na umaarufu aliwageuka na kuanza kuwatukana yeye na baba yake "Kabla sijakukata kichwa Bobi Wine rudisha pesa zetu tulizokukopesha".

Aidha, aliandika akisema "Umeshtushwa na hilo? Sijaanza hata Kabobi (akimaanisha Bobi Wine) ngoja akimbilie kwa Mzee (Rais Museven) kama kawaida yake...Kwa jinsi ninavyofahamu, Kabobi hafai na hajafikia kugombea nafasi ya juu ya Rais wa Uganda," aliandika Jenerali Muhoozi kwenye ukurasa wake wa X.

Hata hivyo, baada ya majibizano yaliyoendelea katika mtandao wa X kati wa wawili hao katika hatua ya nyingine Jenerali Muhoozi aliandika "Ah, nimechoshwa na hizi tweets. Polisi! Mkamateni Kabobi mara moja! Mshike mpaka umlete kwangu...

"Kabobi, nitakupiga, yeyote utakayejificha nyuma yako! Tamka tena jina langu au la familia yangu nitakuvunja meno yako yote hayo ya nyani!," aliandika Jenerali Muhoozi.




Wananchi mbalimbali wa Israel wakishinikiza serikali ya nchini humo kuharakisha jitihada za kuwarudisha mateka waliowekwa kizuizini na kundi la Hamas huko Gaza. **PICHA: MTANDAO**

## Balozi atumbuliwa kwa kulazimisha wafanyakazi kumnyoa sehemu za siri

**LUSAKA, Zambia**

RAIS wa Zambia, Hakainde Hichilema, amemfuta kazi Balozi wa nchi hiyo nchini Afrika Kusini, Mazuba Monze, baada ya madai ya kuwaamrisha wafanyakazi wake wa kiume wamnyoe sehemu zake za siri.

Mwanadiplomasia huyo ambaye alikuwa akihudumu katika ubalozi wa Zambia mjini Pretoria alielezwa kuwa alitoa maagizo kwa wafanyakazi wake ambayo ni kinyume na matakwa ya kidiplomasia, na kwamba wafanyakazi hao walikataa, wakisema kuwa haikuwa sehemu ya majukumu yao kumnyoa balozi hasa sehemu za siri.

Ilielezwa kuwa baada ya watumishi hao kugoma kutekeleza agizo hilo, Balozi Mazuba alichukulia kitendo hicho kuwa ni kutotii na hivyo kuwafuta kazi wafanyakazi hao. Hata hivyo, baada ya ukimya wa muda mrefu wafanyakazi walikata rufani dhidi ya uamuzi huo na kulifikisha suala hilo kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Wakati madai kuhusu matakwa hayo yaliyoshangaza wengi ya Mazuba yalipothibitishwa, Rais Hichilema alimfuta kazi mara moja balozi huyo wakati huo huo ripoti nyingine zikisema kuwa madai dhidi ya balozi huyo yametiwa chumvi.

Gazeti la Maravi Post liliandika kuwa raia wa Zambia anayeishi Afrika Kusini amejitokeza, akidai kuwa madai dhidi ya mwanadiplomasia huyo huenda yametiwa chumvi au kutungwa na wapinzani wake, akidai kuwa kampeni ilizinduliwa dhidi ya Mazuba, ikihusisha ripoti za uongo na uzushi, ambao hatimaye ulisababisha kufukuzwa kwake.

Wakati hayo yakiendelea, bado inabakia kusuburiwa ni hatua gani zaidi zitachukuliwa na matokeo gani balozi huyo atakabiliana nayo, huku ikielezwa kuwa tukio hilo limeacha doa kwa sifa ya kidiplomasia ya Zambia na kuibua maswali juu ya mwenendo wa wawakilishi wake nje ya nchi.

# Trump kusomewa hukumu kabla ya kuapishwa

**NEW YORK, Marekani**

JAJI katika mahakama ya New York Juan Merchan anayesikiliza kesi ya utoaji hongo dhidi ya rais mteule wa Marekani Donald Trump anatarajiwa kutoa uamuzi juu ya kesi hiyo siku 10 kabla ya kuapishwa kwake Januari 20, mwaka huu.

Jaji Merchan alisema kupitia taarifa yake kwamba Trump, ambaye ni rais wa kwanza wa zamani kuwahi kuhukumiwa kwa uhalifu, anaweza kujitokeza ana kwa ana au kwa njia ya mtandao katika hukumu iliyopangwa kusomwa Januari 10, mwaka huu.

Ilielezwa kuwa katika uamuzi wa kurasa 18, Jaji Merchan alikataa hoja mbalimbali za mawakili wa Trump wakitaka hukumu yake kutupiliwa mbali.

Jaji huyo alibainisha kwamba hana nia ya kutoa adhabu ya kifungo jela, badala yake anaegemea katika kuachiliwa bila masharti, hukumu nyepesi ambayo hata hivyo itamfanya Trump aingie Ikulu ya White House kama mhalifu aliyepatikana na hatia.

Wakati hayo yote yakijiri, ilibainishwa kwamba mteule huyo wa kiti cha urais Marekani anatarajiwa kukata rufaa ambayo inaweza kuchelewesha kusomwa kwa hukumu yake.

Ilielezwa kuwa Trump alipatikana na hatia huko New York mwezi Mei kwa makosa 34 ya kughushi rekodi za biashara ili kuficha malipo ya pesa kwa nyota wa filamu za ngono Stormy Daniels kabla ya uchaguzi wa 2016.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa mawakili wa Trump walikuwa wakitaka kesi hiyo itupiliwe mbali kwa misingi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uamuzi wa kihistoria wa Mahakama ya Juu mwaka jana kwamba marais wa zamani wa Marekani wana kinga ya kushtakiwa kutokana na vitendo vya kiofisi vilivyofanywa wakiwa madarakani. Vilevile, Jaji Merchan alikataa hoja hiyo lakini alibainisha kuwa Trump hataweza kushtakiwa mara tu atakapoapishwa kama rais.

Msemaji wa Trump, Steven Cheung alishutumu uamuzi wa Jaji Merchan wa kutoa hukumu kwa rais huyo wa zamani, akiuita "ukiukaji wa moja kwa moja wa uamuzi wa kinga ya Mahakama ya Juu na sheria zingine za muda mrefu".

"Kesi hii ya uvunjaji sheria haikupaswa kamwe kuletwa na katiba inataka itupiliwe mbali mara moja," alisema Cheung katika taarifa yake.

Pia Cheung alisema hakupaswi kuwepo na hukumu, akieleza kuwa rais mteule Trump ataendelea kupigana dhidi ya udanganyifu huo hadi utakapokoma.

Trump pia alikabiliwa na kesi mbili za shirikisho zilizoletwa na wakili maalum Jack Smith lakini zote mbili zilitupiliwa mbali chini ya sera ya muda mrefu ya kutomshtaki rais aliyekuwa mamlakani.

Katika kesi hizo, Trump alishutumiwa kwa kula njama ya kutengua matokeo ya uchaguzi wa 2020 aliyoshindwa na Joe Biden na kuondoa idadi kubwa ya nyaraka za siri baada ya kuondoka Ikulu ya Marekani.

**DW**

# BODI YA LIGI ZANZIBAR KUJIFUNGIA KUJADILI RATIBA, MICHUANO CHAN

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MTENDAJI Mkuu wa Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Issa Kassim, amesema bado hawajakutana ili kujadili kwa pamoja iwapo Ligi za Zanzibar zitasimama kupisha michuano ya Wachezaji Wanaocheza Soka la Ndani (CHAN) ama zitaendelea.

Akizungumza na gazeti hili jana. Kassim alisema bodi hiyo inatarajia kukutana mapema wiki hii kujadili ratiba ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar pamoja na Ligi Daraja la Kwanza Kanda hasa katika kipindi hiki cha kuelekea michuano ya CHAN.

Alisema kikao hicho kwa hatua ya awali kitashirikisha viongozi wa Klabu za Ligi Kuu Zanzibar pamoja na zile za Kanda kabla ya Kamati Tendaji ya ZFF kukutana na kushirikisha serikali kupitia wizara yenye dhamana ya michezo visiwani hapa.

Mtendaji Mkuu huyo alisema baada ya kikao hicho ndipo Bodi ya Ligi hiyo itatoa taarifa rasmi kwa vyombo vya habari kuelekea ratiba ya mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Zanzibar na ile ya Daraja la Kwanza Kanda.

"Kwa sasa siwezi kusema kitu chochote kuelekea ratiba ya mzunguko wa lala salama, kama tunavyojua kuna mashindano ya CHAN ambayo Tanzania ni mwenyeji, hivyo tutatoa taarifa hapo baadaye," alisema.

Aidha, alisema mbali na michuano hiyo ya CHAN lakini pia watajadili viwanja vya kucheza Ligi Kuu kutokana na wanavyovitumia kwa sasa vyote vipo katika matengenezo.

"Uwanja wa Amaan bado upo katika matengenezo, Uwanja wa Mau pia hivyo hivyo, hivyo basi lazima katika vikao tuone uwanja gani ambao utatumiwa kucheza mzunguko wa pili ikiwa ligi itaendelea," alisema.

Kwa sasa ligi zote Zanzibar zimesimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi ambayo inaendelea Kisiwani Pemba.

KIKAPU...



Vijana wakifanya mazoezi ya mpira wa kikapu katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wachezaji Mbeya City waitaka Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Mbeya City wameahidi kuendelea kupambana kwenye michezo ya Ligi ya Championship ili kuipandisha Ligi Kuu msimu ujao na kutekeleza kaulimbiu ya klabu hiyo na mashabiki wake iliyozinduliwa wiki hii, isemayo 'Tunaitaka Ligi Kuu.'

Wakizungumza kutoka Mbeya, wachezaji wa timu hiyo, Kilaza Mazoea na David Mwasa, wamesema msimu huu wamedhamiria kuipandisha timu hiyo Ligi Kuu, licha ya kwamba wanakabiliana na ugumu wa Ligi ya Championship.

"Wachezaji wote tumeambizana kuwa tunachohitaji ni kushinda mechi zijazo ili tupande Ligi Kuu, tunajua Ligi ya Championship nayo ni ngumu, lakini tunapambana.

"Malengo ya klabu na mashabiki wetu mwaka huu timu irejee Ligi Kuu na ndiyo maana wana kaulimbiu msimu huu isemayo, 'Tunaitaka Ligi Kuu', na tunaitaka kweli," alisema Kilaza, ambaye alifunga 'hat-trick' kwenye mchezo ambao Mbeya City iliichabanga Geita Gold mabao 4-0 hivi karubuni.

Naye David Mwasa, alisema kuipandisha Ligi Kuu timu ya Mbeya City kuna faida kubwa, kwani licha ya kwenda kuleta ushindani, lakini wachezaji watapata fursa ya kuonekana vipaji vyao na kupata malisho mazuri zaidi.

"Hii Mbeya City ilishawahi kupanda Ligi Kuu, ilizalisha wachezaji wengi sana, kina David Rafael Loti, Peter Mwalyanzi, Deus Kaseke, Hassan Mwasapili, na wengine wengi ambao walichukuliwa na timu kubwa.

"Ndani ya kikosi kuna vipaji ambavyo huku bado havionekani vema, lakini tukipanda kila mmoja atawaona," alisema Mwasa.

Mara ya kwanza Mbeya City ilipanda Ligi Kuu na kuanza kucheza kwa mara ya kwanza msimu wa 2013/14, kabla ya kuteremka msimu wa 2022/23, ikifungwa na Mashujaa FC kwenye mechi za 'play off.'

Timu hiyo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi ya Championship, ikifikisha pointi 31 kwa michezo 14 iliyocheza, ikiwa nyuma ya Mtibwa Sugar yenye pointi 35.

# Tabora United yamulika mbali Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United imetabiri kuwa mechi zao za mzunguko wa pili zitakuwa ngumu zaidi kuliko za kwanza kwani timu nyingi zitakuja kwa tahadhari na zingine kucheza kwa kukamia dhidi yao.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Christina Mwagala, amesema kiwango bora ambacho imeonesha timu hiyo katika mechi za mzunguko wa kwanza, kimeonekana kuwashangaza wengi na sasa wanaitolea macho na kuiona si timu ya kwenda kucheza nayo bila kugangamala.

Kutokana na hilo, amesema wamewapa mapumziko ya muda mfupi tu wachezaji wao, kabla ya kuanza tena mazoezi ili kuwafanya wasipoteze uwezo wao waliouonesha awali.

"Tumewapa mapumzuko ya muda mfupi tu wachezaji wetu na watarejea tena kwenye mazoezi kwa sababu hatutaki wakae sana na mzunguko wa pili waonekana kama wanaanza upya.

"Kwa kile tulichoonesha mzunguko wa kwanza, tunaamini kabisa kuwa sasa timu zote zitakuja kwa tahadhari na zingine kukamia zikicheza na sisi kwa sababu zitajua zinakwenda kucheza na timu bora. Hazitokuja kama ambavyo zilifanya kwenye mzunguko wa kwanza ambapo walikuwa wanatuchukulia poa, badala yake kila atakayekuja kucheza na sisi atakuja kwa kujikaza na kukamia zaidi ili kuhakikisha haipotezi dhidi yetu," alisema Mwagala.

Alisema kwa kutambua hilo, wametoa mapumziko mafupi tu, lakini pia wataongeza ubora kwenye kikosi chao ili kuendelea kuwa timu ya kutisha, kwani wanaamini timu nyingi zitafanya usajili kipindi hiki cha dirisha dogo.

"Itakuwa ni duru ya lala salama, kila timu itakuja ikiwa imefanya usajili wa kuziba mapungufu yaliyoonekana, kwa hiyo haitokuwa rahisi. Ligi Kuu msimu huu ni ngumu na bora sana kwa hiyo na sisi ni lazima tujipange, tumekuwa moja ya timu zinazoangaliwa sana, tumeifunga Yanga, Azam na kutoka sare na Singida Black Stars, kwa sasa tupo nafasi ya tano tukiwa na pointi 25, tuaahidi na sisi tutarudi tukiwa imara kuliko mzunguko wa kwanza, tunataka kuendelea kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema Ofisa Habari huyo.

## ZISIKUPITE

### NUNEZ KUWEKWA SOKONI

LIVERPOOL ipo tayari kupokea ofa ya pauni milioni 50 hadi 60 ili kumuuza mshambuliaji wao wa miaka 25 raia wa Uruguay, Darwin Nunez. ***(Football Insider)***

### RASHFORD AWANIWA MILAN

AC Milan imeibuka kuwa klabu ya hivi karibuni inayofikiria kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, 27. ***(Mail)***

### WEST HAM NA WASHAMBULIAJI

WEST Ham inaandaa orodha ya washambuliaji inapopania kuwasajili Januari hii ikiwajumuisha mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye miaka 20, mshambuliaji wa Wolves na Korea Kusini, Hwang Hee-chan (28) na mshambuliaji wa Middlesbrough raia wa Ivory Coast, Emmanuel Latte Lath, 26. ***(Telegraph)***

### CUNHA KUONGEZA MKATABA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Matheus Cunha mwenye miaka 25, anakaribia kusaini mkataba mpya ulioboreshwa katika Klabu ya Wolves licha ya Arsenal kumtaka. ***(Telegraph)***

### MUANI AWANIWA BAYERN

RANDAL Kolo Muani huenda akaondoka Paris St-Germain mwezi huu, huku AC Milan, Juventus, Bayern Munich, RB Leipzig, Aston Villa na Tottenham Hotspur zikimwania mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26. ***(Ben Jacobs)***

### CASADEI KUTUA TORINO

KIUNGO wa Chelsea, Cesare Casadei amekubali dili la kujiunga na Torino inayoshiriki Ligi Kuu ya Italia, Serie A. ***(Gianluca di Marzio)***

### OSIMHEN KUBAKI GALA

KLABU ya Galatasaray inaimani kwa asilimia 100 kwamba mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 26, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu hiyo kutoka Napoli, hataondoka Uturuki Januari hii. ***(Florian Plettenberg)***

### OLMO ATAKIWA MILAN

AC Milan inataka kumsajili Dani Olmo wa Barcelona kwa mkopo wa miezi sita ingawa mshambuliaji huyo wa Hispania mwenye miaka 26, hapatikani kwa sasa kutokana na vikwazo vya usajili wa LaLiga vilivyowekwa dhidi ya Barca. ***(Corriere della Sera, via Sport)***

### WINDASS AWINDWA SANTOS

KLABU ya Santos ya Brazil imewasilisha ombi la kutaka kumsajili kiungo wa England, Josh Windass mwenye umri wa miaka 30, kutoka Sheffield Wednesday. ***(TalkSport)***

### JABER ANYATIWA

SWANSEA City ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ulaya zinazomwania kumnunua kiungo wa Saudi Arabia, Abdulmalik al-Jaber mwenye umri wa miaka 20, anayechezea timu ya Zeljeznicar nchini Bosnia. ***(TeamTalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES AKUNWA NA KIWANGO UTD KWA LIVER

**Kwa nini hatuwezi kufanya hivi kila wiki? Nimesikitishwa sana kwa sababu...**

**Manchester, England**

NAHODHA wa Manchester United, Bruno Fernandes, amesema yeye na wachezaji wenzake hawajaridhika licha ya kupata sare dhidi ya vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool.

Fernandes alitoa pasi ya bao la ufunguzi la Lisandro Martínez katika sare ya mabao 2-2 na alitangazwa mchezaji bora wa mechi.

Hatua hiyo inawapa United na Kocha Mkuu, Ruben Amorim, ahueni inayohitajika baada ya kufungwa mara nne mfululizo katika michuano yote, ikiwa ni pamoja na kupoteza dhidi ya Newcastle United, Wolverhampton Wanderers na Bournemouth.

"Nimesikitishwa sana kwa sababu tulionesha kiwango bora hii leo (juzi) dhidi ya Liverpool, kwa nini hatuwezi kufanya hivi kila wiki?" alisema Fernandes akiiambia Sky Sports baada ya mchezo.

"Tulisema kabla ya mchezo, tunahitaji mengi zaidi kutoka kwetu ili kupata kitu msimu huu. Tunahitaji kuangalia mbele. Tunahitaji zaidi.

"Sikuwa na wasiwasi kuhusu watu kuweka juhudi kwa sababu ni Liverpool, kila mtu atajaribu kufanya bora kwake.

"Leo (juzi) ilikuwa ni kuweka bidii kwenye mchezo, kucheza kwa shauku," aliongeza Fernandes.

"Una mbinu, lakini mwisho wa siku unahitaji kuweka juhudi na ndiyo maana tumepata kitu kwenye mchezo huu.

Mechi inayofuata ya United itacheza na Arsenal katika Uwanja wa Emirates Jumapili ijayo kwenye Kombe la FA raundi ya tatu.

Mchezo wa nyumbani dhidi ya Southampton unafuatia, United ikiwa nafasi ya 13 kwenye ligi baada ya mechi 20.



# Chelsea kusaka beki Januari hii

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Enzo Maresca, alidokeza kushinikiza kuimarishwa kwa safu ya ulinzi wakati wa uhamisho wa Januari hii baada ya timu yake kutoka sare ya bao 1-1 na Crystal Palace Jumamosi.

'The Blues' wameshindwa kushinda mechi zao nne zilizopita, wakitoka sare na Everton na Palace.

Maresca alikuwa ameongoza ushindi mara nane mfululizo kabla ya matokeo mabaya katika kipindi cha sikukuu, ambayo yameambatana na wingi wa majeraha katika safu ya ulinzi.

Wakati nahodha wao Reece James amerejea kwenye kikosi cha Chelsea hivi karibuni - lakini bado hajacheza mechi yake ya kwanza tangu Novemba - ilithibitishwa kuwa beki wa kati Wesley Fofana atakuwa nje kwa kuumia msuli wa paja.



Benoit Badiashile pia atakuwa nje ya uwanja hadi mwezi ujao, na kumuacha Maresca akikosa nafasi kwenye safu ya ulinzi - kama alivyosema baada ya matokeo mabaya ya Jumamosi. "Labda kutokana na majeraha ya Wes na Benoit, tutaona kama kuna kitu kitatokea," alisema kocha huyo raia wa Italia.

Huku beki mahiri Renato Veiga akiwa njiani kuelekea Serie A, The Blues wanaweza kufungua nafasi katika bajeti kwa ajili ya mchezaji mpya - na anayehitajika sana - safu ya ulinzi.

# Rashford atakiwa AC Milan

**MILAN, Italia**

VIGOGO wa Ligi Kuu Italia, Serie A, AC Milan wanafikiria kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, kwa mkopo.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa England yupo kwenye uvumi wa uhamisho tangu alipofichua nia yake ya "changamoto mpya" katikati ya Desemba.

Ruben Amorim tayari alikuwa amemtoa Rashford katika mchezo wa dabi ya Manchester mwezi uliopita wakati alipotoa kauli hizo za msisitizo, na hivyo kuzua uvumi kwamba anaondoka.

Wakati Amorim akiendelea kusisitiza kwamba Rashford anaweza kurejea kwenye kikosi cha kwanza cha United, klabu hiyo imeripotiwa ipo tayari kumuuza mhitimu huyo wa Akademi ya Man United.

Na sasa Milan inadhaniwa kuvutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Kikosi hicho cha Serie A kilibadilisha kocha hivi karibuni na kumleta Sergio Conceicao wa Ureno kuchukua nafasi ya Paulo Fonseca mwanzoni mwa wiki.

Dirisha la Januari sasa limefunguliwa na United wako tayari kupokea ofa yoyote ya mkopo ambayo inajumuisha kipengele cha wajibu wa kumnunua moja kwa moja.

Baadhi ya ripoti zinaonesha kuwa upande wa Amorim utakubali ada ya chini kama pauni milioni nne katika jitihada za kuondoa mshahara wa Rashford - ambao ni pauni 325,000 kwa wiki.

# RONALDO HANA MPANGO WA KURUDI TENA ULAYA

**RIYADH, Saudi Arabia**

CRISTIANO Ronaldo amesema anaangalia yanavyokwenda akiwa na Al Nassr, na kuondoa uwezekano wa uhamisho wa kushtukiza Januari hii.

Ronaldo, ambaye anatimiza umri wa miaka 40, Februari, alihamia Saudi Arabia mwaka 2023 baada ya kuwa na wakati mgumu Manchester United, huku akisaini mkataba mnono wa miaka miwili na nusu.

Mkataba huo wenye thamani ya pauni milioni 177 unatarajiwa kumalizika msimu huu wa majira ya joto, na hivyo kuzua uvumi kwamba mfungaji huyo bora zaidi katika historia ya soka ya kimataifa ya wanaume huenda anatazamia kurejea Ulaya.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City - wapinzani wakubwa wa Man United - wametajwa kuwa mahali pa kushtukiza kwa Ronaldo, huku pia Paris Saint-Germain nayo ikitajwa.

Lakini Ronaldo, ambaye anaendelea kung'ara akiwa na Al Nassr, amesema ataheshimu mkataba wake aliosaini Januari 2023, huku akitilia mkazo katika kusaidia timu hiyo kushinda mataji.

Ronaldo aliviambia vyombo vya habari vya Saudia: "Nina furaha na familia yangu ina furaha. Tulianza maisha mapya katika nchi hii nzuri. Maisha ni mazuri, soka ni zuri. Kwa upande wa mtu binafsi na wa pamoja, bado tupo hapa.

"Ni vigumu kushindana na timu kama Al Hilal na Al Ittihad, lakini bado tupo, bado tunasukumana na kupigana. Soka ni hivyo; una wakati mzuri na wakati mbaya.

"Lakini, kwangu, jambo muhimu zaidi ni kuwa naendelea kucheza hapa kwa bidii, kuheshimu klabu, kuheshimu mkataba na kuamini kwamba mambo yatabadilika - kwa Al Nassr kujaribu kushinda mataji

HABARI MICHEZO

# BALEKE SASA MBIONI KUTUA NAMUNGO FC

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa Yanga, Jean Baleke, imeelezwa yupo kwenye mazungumzo na klabu yake ili iweze kumruhusu kwenda Namungo FC, jambo ambalo linaweza kukamilika kwa urahisi kutokana na mchezaji huyo kukosa namba kwenye kikosi hicho.

Habari zilizopatikana jana kutoka ndani ya Klabu ya Namungo, zinasema wameshaongea na mchezaji mwenyewe na kukubaliana kutua, lakini kwa sababu bado ana mkataba wa mwaka mmoja na nusu uliobaki, wamebisha hodi kwa ajili ya kuona kama anaweza kupatikana kwa mkopo.

„Kama mambo yatakwenda vizuri tunamhitaji kwa mkopo wa mwaka mmoja, nadhani mambo yatakwenda vizuri tu kwa sababu yeye mwenyewe hana furaha kwenye kikosi cha Yanga.

„Hapati muda wa kucheza, akija kwetu atatusaidia sana kwa sababu tunaamini bado ana uwezo mkubwa wa kupachika mabao, na tumemwahidi kuwa yeye ndiye atakuwa straika namba moja," kilisema chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo.

Taarifa zinaeleza kuwa straika huyo pia amewaomba mabosi wake wamruhusu kwenda kuitumikia Namungo ili aendeleze kipaji chake kutokana na kukaa muda mrefu bila kucheza.

Baleke, ambaye alikuwa hapati namba chini ya kocha aliyeondoka, Miguel Gamondi, lakini pia hata kocha wa sasa, Sead Ramovic, amekuwa hamtumii kwenye kikosi chake.

Mchezaji huyo aliichezea Simba mwaka 2023, kabla ya kwenda Al Ittihad ya Libya mwaka jana, na kisha kutua Yanga msimu huu.

Siku chache zilizopita, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alibainisha kuwa Beleke hakuwa kwenye mipango ya mwalimu wao.

„Mchezaji Baleke hayupo kwenye orodha ya majeruhi, hayupo kwenye programu ya mazoezi, utaratibu wake upo kwenye Ofisi ya Mtendaji Mkuu, ukikamilika tutawatangazia," alisema Kamwe.

Mbali na Baleke, Namungo ambayo kwa sasa inafundishwa na Juma Mgunda, pia ipo katika mazungumzo na Klabu ya Simba juu ya kumsajili winga, Selehe Karabaka, kwa nia ya kukiongezea kikosi nguvu kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa imesimama kupisha Kombe la Mapinduzi na michuano ya Mataifa ya Afrika Wachezaji wa Ndani, CHAN.

MCHANGANI....



Vijana wakifanya mazoezi ya kucheza mpira katika Uwanja Mchanga wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ndemla, Ambundo hatari kwa 'fri-kiki' Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa JKT Tanzania, Said Hamisi Ndemla, na winga wa Fountain Gate, Dickson Ambundo, wanaongoza kwa kufunga mabao mengi ya mikwaju ya faulo ya moja kwa moja katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, wachezaji hao kila mmoja, amefunga mabao mawili kwa faulo za moja kwa moja walizopiga kuelekea kwa wapinzani wao.

Wakati Ndemla aliwahi kuichezea Simba, Ambundo amewahi kuwa machezaji wa Yanga misimu kadhaa nyuma.

Nyota hao wanafuatiwa na wachezaji watano ambao kila mmoja amefunga faulo moja kwenye ligi mpaka sasa.

Wachezaji hao ni Clatous Chama wa Yanga, Jean Ahoua wa Simba, Redemtus Mussa wa KMC, Salum Kihimbwa wa Fountain Gate na Ezekia Mwashilindi wa Prisons.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo Nipashe, Chama alifunga faulo yake, Oktoba 22, mwaka jana dhidi ya JKT Tanzania, katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Simba ikishinda mabao 2-0.

Ahoua, alifunga bao lake la faulo, Desemba 21, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera wakati timu yake ya Simba ikitoa kichapo cha mabao 5-2.

Kwa upande wa ‚clean sheets' bado kipa, Moussa Camara wa Simba anaendelea kusumbua, akiwa nazo 12 mpaka sasa.

Wakati Camara akiendelea kuwatesa makipa wa Ligi Kuu kwa ‚clean sheets', anayefuatia ni Patrick Munthali wa Mashujaa FC ambaye ana nane mpaka sasa.

Makipa wanaoshika nafasi ya tatu kwa kukaa michezo mingi bila wavu wao kugushwa ni, Djigui Diarra wa Yanga, raia wa Mali, na Metacha Mnata wa Singida Black Stars ambao wana ‚clean sheets' saba kila mmoja, huku Mohamed Mustafa wa Azam FC, raia wa Sudan akiwa nazo sita.

Makipa wengine ni Yacoub Suleiman wa JKT Tanzania na Yona Amosi wa Pamba Jiji, ambao wamekaa langoni bila kuruhusu wavu kugushwa mara tano kila mmoja mpaka sasa.

## Fadlu: Tutafuzu robo fainali tukiwa Angola

INATOKA UK. 24

kadhaa iliyopita.

Mfungaji wa bao hilo pekee, kiungo mshambuliaji raia wa Ivory Coast, Jean Charles Ahoua, alisema mchezo ulikuwa mgumu kwani walizihitaji mno pointi tatu, lakini sasa wanaangalia michezo iliyobaki.

"Tuna furaha kwa ushindi huu kwa sababu mechi ilikuwa ngumu sana, tulihitaji pointi tatu kwa njia yoyote ile kwa ajili ya kujiweka kwenye sehemu nzuri ili kuweza kufuzu, tuna furaha na mimi nina furaha kwa kuipatia timu yangu ushindi.

"Pamoja na hayo, tunapaswa sasa kuangalia michezo miwili iliyobaki, hasa dhidi ya Bravo do Maquis, ambayo tukifanya vema tutakuwa tumefuzu," alisema.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Murtaza Mangungu, aliwasifu wachezaji kwa kupambana licha ya ugumu wa hali ya hewa.

„Hali ya hewa ilikuwa ngumu sana, ni baridi sana, pamoja na kwamba timu ilikuja mapema kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa, lakini hali haikuwa nzuri sana.

"Tunashukuru kocha Fadlu Davids kwa kutengeneza ‚plan' nzuri ya uchezaji, wachezaji nao wamejituma kwa kiasi kilichostahili na kuweza kuwadhibiti, wenzetu walikuwa wanacheza wakisema liwalo na liwe ni lazima wapate ushindi, na sisi tulihitaji ushindi pia," alisema.

Simba inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi tisa sawa na CS Constantine inayoongoza, lakini inazidiwa kwa tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa, Bravo do Maquis ikiwa na pointi sita, nafasi ya tatu, CS Sfaxien ikiburuza mkia bila pointi.

## Mzize atabiri bao lake bora Afrika

INATOKA UK. 24

sana," alisema Mzize.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ameweka wazi mbinu aliyoifanya hadi kuifunga TP Mazembe na kuchupa hadi nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi ya Mabingwa Afrika Kundi A, ikifikisha pointi nne.

„Kwa sasa tunacheza kwa kasi, tunakimbia pamoja, hakuna beki, mshambuliaji wala kiungo, kila mmoja anapaswa kukimbia mbele au nyuma na kumnyima mpinzani nafasi kwenye wakati sahihi.

Tuna wiki nne sasa tumekuwa imara, wachezaji wangu wamekuwa na nidhamu na kujituma, hicho ndicho kilichoikuta TP Mazembe na isingeweza kukiepuka kipigo kwa namna yoyote, hata timu zingine pia nadhani hazitotuonea tena kama ilivyokuwa awali," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Wakati Yanga ina pointi nne, MC Alger ya Algeria, juzi ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan, matokeo ambayo yamewafanya Waalgeria hao kubaki nafasi ya pili kwa kufikisha pointi tano, Al Hilal ikiendelea kuongoza kwa pointi 10.

# Michezo

Jumanne Januari 7, 2025

Nipashe


Fernandes akunwa na kiwango Utd kwa Liver

UKURASA 21



MWAMBA HUYU HAPA...



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Charles Ahoua, akiachia shuti kali lililojaa kimyani licha ya kuzongwa na beki wa CS Sfaxien, katika mechi ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi jijini Tunis, Tunisia juzi na kuiwezesha timu yake kushinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

# Fadlu: Tutafuzu robo fainali tukiwa Angola

●●● Ataka mechi ya mwisho kwa Mkapa wacheze kama Tamasha la Simba Day, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema kazi iliyobaki ni kuhamishia majeshi yake nchini Angola dhidi ya Bravos do Maquis, akisema anataka timu yake ifuzu hatua ya robo fainali ikiwa nchini humo, ili mechi ya mwisho dhidi ya CS Constantine ya Algeria iwe kama Tamasha la Simba Day.

Akizungumza nchini Tunisia baada ya kumalizika kwa mchezo wa raundi ya nne, Kombe la Shirikisho Afrika uliochezwa Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi jijini Tunis na kushinda bao 1-0 dhidi ya CS Sfaxien ya nchini humo, alisema katika mchezo huo utakaopigwa Jumapili ijayo, watahakikisha wanafanya kila njia ili wafuzu kwani wanahitaji ushindi au sare tu.

Alisema haitokuwa rahisi, lakini atakiandaa kikosi kucheza kama fainali katika mchezo huo.

"Tumefurahi, tumeshinda mchezo huu muhimu kwa sababu ulikuwa ni lazima, baada ya hapa kilichobaki ni kwenda Angola tukiwa na kazi moja tu ya kutinga hatua ya robo fainali tukiwa kwenye ardhi hiyo, kwa bahati nzuri tunahitaji matokeo mawili, ushindi au sare.

Ushindi utatufanya tufikishe pointi 12, na sare tutakuwa na pointi 10, tutanufaika na kanuni ya sisi na Bravo do Maquis tulipokutana, kwani hata kama akishinda mchezo wa mwisho dhidi ya CS Sfaxien na kufikisha pointi 10, sisi tutasonga mbele hata kama tutapoteza mechi ya mwisho," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, Fadlu alisema kwa malengo ya awali aliyojiwekea kikosi chake kingekuwa kimeshafuzu mpaka sasa.

Alisema alihitaji pointi 10 hadi 12 awe nazo mpaka sasa, lakini kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Constantine nchini Algeria, kilitibua mipango na malengo yote aliyojiwekea.

"Nilihitaji hadi muda huu tuwe na pointi 10 au 12, baada ya mechi nne, hatukutaka kupoteza hata mchezo mmoja kwenye kundi hili, hesabu zilivurugika baada ya kufungwa na CS Constatine, pamoja na hayo tutahakikisha hatupotezi mchezo wowote ule kati ya miwili iliyobaki," alisema Fadlu.

Aliwasifu wachezaji wake kwa kucheza kwa maelekezo, kwani waliwajibika uwanjani huku wakikabiliwa na hali ya hewa ya baridi ambayo hawakuizoea zaidi ya wapinzani wao, lakini pia kupunguza makosa binafsi ambayo yaliwaathiri kwenye michezo

INAENDELEA UK. 23

## Mzize atabiri bao lake bora Afrika

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Clement Mzize, amefunguka kuwa hajawahi kufunga bao bora na zuri katika historia yake ya soka kama alilolifunga katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, uliochezewa Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mzize, ambaye alipachika mabao mawili katika mchezo huo hatua ya makundi, moja likiwekwa wavuni na Stephane Aziz Ki, alisema bao la kusawazisha alilolifunga dakika ya 33, linaingia kwenye kumbukumbu ya bao namba moja kwa ubora kati ya yote aliyoyafunga, huku akitabiri kuwa huenda likaingia kwenye kinyang'anyiro cha bao bora na kushinda.

Straika huyo ambaye anaichezea pia Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, aliupata mpira karibu na katikati ya uwanja, upande wa Mashariki ya Uwanja, akaanza kuukokota bila kubugudhiwa na mchezaji yeyote, alivyoona hivyo aliamua kuachia shuti kali la mbali, umbali wa takriban yadi 35 na kwenda kujaa juu ya maungio ya mwamba wa juu na nguzo ya chini, huku kipa, Alioune Badara Fatty, akiruka bila mafanikio.

Lilikuwa ni bao la kusawazisha baada ya kufungwa la kwanza na kipa Badara, dakika ya 16 kwa mkwaju wa penalti.

„Sijawahi kufunga bao kama lile, ni mara ya kwanza tangu nianze soka, hata huko mchangani ambako sijawahi kuonekana sikufunga bao la namna ile hata mara moja.

„Nimewahi kufunga mabao, lakini si kama lile, ni bao ambalo limeingia kwenye historia yangu, awali niliona la kawaida tu, mechi ilivyoisha kila mtu nasikia analizungumzia, ikabidi na mimi niende kuliangalia upya, ni bao zuri, huwezi kujua, linaweza kuingia katika orodha ya mabao bora Ligi ya Mabingwa Afrika au likashinda kabisa, tuombe Mungu, inawezekana likawa bao bora Afrika," alisema Mzize.

Kuhusu bao la pili alisema halikuwa na maajabu sana kwa sababu ni vitu ambavyo huwa wanavifanyia kazi mazoezini.

"Bao la pili nililofunga ni vitu ambavyo tumekuwa tukivifanya mazoezini ni kama vinajirudia tu, yale tunafunga

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >